




**Mganga** Mkuu asimamishwa kazi madai wizi wa mafuta

UKURASA 3

TUNANUNUA BETRI CHAKAVU ZA ASID

JE, BETRI LAKO LIMEHARIBIKA? TUUZIE: TUNANUNUA MABETRI YALIYOHARIBIKA



Sisi ni Wanunuzi wazuri wa Betri za Asidi zilizoharibika kuweza kutumika tena. Tunatoa suluhisho juu ya njia nzuri za kuteketeza/kuhifadhi betri za Asidi zilizotumika. Tupo ndani ya Dar-es- Salaam.

Kama unazo Betri zilizotumika au kwa mahitaji mengine, tafadhali wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo hapo chini:

Gaia Eco Solutions (T) Ltd
P.O. Box 40144, Dar-es-salaam.
Cell: +255-689 051591
Email: gaia.scrap@synarge.com

Nipashe

Jumatatu Mei 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580954

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

TOZO MAFUTA

# Wadau usafirishaji, wachumi wafunguka

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### SERIKALI YALETA TOZO MPYA KIGAMBONI

SERIKALI imefanya mabadiliko ya tozo za kuvuka katika daraja la Kigamboni, jijini Dar es Salaam, kwa kuweka utaratibu mpya utakaoruhusu mtu kulipa kwa safari, siku, wiki...

UKURASA WA 4

### MWALIMU MKUU JELA KUGHUSHI FEDHA UJENZI

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Mwenge wilayani Rorya mkoani Mara, Issaya Gwidana, amehukumiwa kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya Shilingi milioni mbili baada...

UKURASA WA 4

### MO DEWJI ATUNUKIWA PHD NCHINI MAREKANI

MFANYABIASHARA bilionea Mohammed Dewji maarufu MO, ametunukiwa udaktari wa falsafa (PhD) na Chuo Kikuu cha Georgetown McDonough School of Business cha...

## Polisi yazingira ofisi za NCCR Dar

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa, akiendesha kikao maalum cha Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, jana Chamwino, jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sekta binafsi kuzalisha ajira mpya milioni nane

UKURASA 2

MICHEZO NABI AANZA MSAKO USAJILI MPYA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza na wadau wa utalii wakati wa kongamano lililofanyika jijini Arusha. Benki ya NMB iliwakutanisha wadau wa utalii zaida ya 150 ili kujadili mbinu za kuboresha biashara zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TOZO MAFUTA

# Wasafirishaji, wachumi wafunguka

**Na Jenifer Gilla**

WASAFIRISHAJI, wachumi na wananchi wamepongeza ahadi iliyotolewa na serikali ya kuweka ruzuku na kuondoa au kupunguza kodi na tozo mbalimbali kwenye mafuta ili kuleta nafuu kwenye maisha ya wananchi.

Hivi karibuni serikali ilitangaza kuweka ruzuku ya Sh. bilioni 100 kwenye mafuta na kurekebisha au kuondoa kodi na tozo mbalimbali katika bajeti ya serikali itakayowasilishwa bungeni na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, Juni 16, mwaka huu.

Msemaji wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Mustapha Mwalongo, alisema wanaziona juhudi hizo kuwa zinakwenda kukabili na kupunguza mfumuko wa bei ya mafuta, na kwamba kwa sasa wamekaa mkao wa kusubiri siku 25 zijazo.

"Juhudi za serikali tunaziona, ndiyo maana unatuona kwa muda sasa tupo kimya, serikali imeamua kutia mkono kama maombi yetu ya awali tuliyozungumza nao tukiitaka iingilie kati ili kuleta ahueni," alisema.

Aliongeza kuwa wanajisikia faraja kuona kuwa serikali imeamua kuyafanyia kazi maombi yao waliyoyatoa na wanaamini kuwa mafuta hayo yatashuka bei ifikapo Juni au Julai, mwaka huu.

"Kwa hiyo tunaiomba serikali iendelee kutia jitihada, juu ya suala la mafuta kwa kuwa katika biashara hii ya usafirishaji mafuta ndiyo uti wa mgongo. Tunaishukuru kwa hapa ilipofikia tunaridhika sana," alisema Mwalongo.

Naye Mwenyekiti wa Daladala Mkoa wa Dar es Salaam, Sabri Mabrouk, alisema wanafurahi kuona serikali inajituma na kwamba wanasubiri ahadi hiyo kwa hamu kwa kuwa wanaamini mafuta yakishuka yatasaidia kurudisha hesabu ya zamani ambayo ilikuwa inatoa faida.

"Unajua sisi wa daladala tulianza kuathirika tangu zile 'level seat' (kutosimama abiria) za kipindi cha corona, hatukupumzika sana ikaja vita ya Ukraine ambayo imesababisha hii adha ya mafuta, kwa hiyo jitihada za serikali kupunguza mafuta ni nzuri na tunazisubiri kwa hamu kwa kuwa bado tunafanya biashara kwa hasara," alisema Mabrouk.

Aliongeza kuwa jitihada hizo za serikali pia zinaonyesha ni jinsi gani inawafikiria wananchi wake kwa kuwa adha hiyo pia imewaathiri watumiaji wa magari hayo hasa wanaopanda daladala.

"Kama unatumia daladala dada yangu utaona jinsi zilivyopungua barabarani kutokana na wamiliki wengi kuamua kulaza magari, hali hii ikiendelea itasababisha usafiri wa abiria kuwa wa shida hivyo kuathiri shughuli za wananchi zinahitaji huduma hii, kwa hiyo tunaishukuru serikali kwa kuliona hili," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Kijamii (ESRF), Dk. Hoseana Lunogelo, alisema kuwa jambo litakuja kwa wakati muafaka kwa kuwa maeneo mengi kutakuwa na shughuli za mavuno, hivyo kushuka kwa bei kutasaidia bei ya vyakula isipande.

"Kwa sasa serikali imefanya jambo kubwa la kuhakikisha kuwa mfumuko hauendelei na baada ya muda tunategemea bei hizo zitashuka hali ambayo inaleta faraja, ukizingatia tunaelekea kipindi cha mavuno sasa bei hizo zikiendelea kupanda hata kupatikana kwa mavuno shambani kusingesaidia kushusha bei ya chakula kwa kuwa gharama za kusafirisha zingekuwa juu," alisema.

"Kuna sekta nyingine zilikuwa bado hazijaambukizwa kwenye hili tatizo la mfumuko, kwa mfano gharama za hospitali, shule sasa kama serikali isingechukua hatua za kusitisha mfumuko wa bei hata huku pia kungekuja kuambukizwa, naipongeza kwa hili," alisema mchumi huyo.

Meneja wa kampuni ya mabasi ya Tashrif, Shabani Shemweta, alisema jitihada za serikali kupunguza bei ya mafuta zitaokoa vijana waliokosa kazi kwa kuwa wamiliki watarudisha mabasi waliopaki kutokana na changamoto hiyo.

"Kuna vijana wamepoteza kazi wapo mitaani wanaumia kutokana na uamuzi wa wamiliki kupunguza ruti za magari ili kufidia gharama za mafuta, sisi tunaishukuru serikali yetu kwa kuendelea kutupigania katika suala la mafuta kwa kuwa bado ni changamoto katika sekta ya usafirishaji. Japokuwa nauli zimepandishwa, lakini bado faida haipatikani kwa sababu hela yote inaishia kwenye mafuta na kulipa dereva na kondakta," alisema.

Kondakta wa daladala zinazokwenda Kawe, Aziz Juma alisema kuwa juhudi zinazofanywa na serikali za kupunguza bei ya mafuta ni za kiungwana na zinaonyesha ni jinsi gani inavyojali watu wake, hasa madereva na makondakta waliopoteza ajira kutokana na wamiliki wa daladala hizo kusimamisha huduma hiyo.

"Yaani dada mimi hapa naisubiri hiyo ahadi ya kushuka kwa bei ya mafuta kwa hamu kwa sababu ninaamini madereva waliopo mtaani watarudi kazini, kwa kweli hii ndiyo serikali tunayoitaka, inayotafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoumiza wananchi," alisema.

Naye Doris Peter, mkazi wa Ubungo External, alisema kuwa jitihada za serikali za kudhibiti na kupunguza mfumuko wa bei ya mafuta ni za kupongezwa kwa sababu wananchi wa hali ya chini ndiyo wanaumia zaidi, kwasasa pikipiki na bajaji zimepandisha bei.

"Kwa kweli mimi huyu mama (Rais Samia) nina mpenda sana, anajua kufikiria watu wake, sisi ambao tunalazimika kupanda bajaji au bodaboda kutokana na umbali wa kufika kituoni tunaiona joto ya jiwe, naitamani sana hiyo siku ambayo bei ya mafuta itatangazwa kuwa imeshuka, ili turudi katika maisha ya zamani, maana sasa kila kitu kipo juu," alisema Doris.

**TOZO/KODI**

Hadi sasa tozo zinazotozwa kwenye mafuta ni ya matumizi ya miundombinu ya bandari inayotozwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), kuchakata nyaraka za forodha ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kupima na kuthibitisha kiwango cha mafuta kinachopokelewa nchini ya Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA).

Kupima na kuthibitisha ubora wa mafuta ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), uwakala wa Meli ya Shirika la Wakala wa Meli (TASAC) na ya shughuli za udhibiti wa biashara ya mafuta ya EWURA.

Aidha, tozo za taasisi za serikali ni matumizi ya bandari, huduma kwenye halmashauri, tozo katika biashara ya jumla na rejareja kwa wakaguzi wa miundombinu, Baraza la Mazingira Tanzania (NEMC), OSHA, Zimamoto, Wakala wa Barabara Tanzania (TANDROADS), Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA).

Mei 10, mwaka huu, Waziri wa Nishati, January Makamba, aliwasilisha bungeni hatua zilizochukuliwa na serikali ili kuleta nafuu.

# Sekta binafsi kuleta ajira mpya milioni 8

**Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itaboresha mazingira ya biashara ili kuiwezesha sekta binafsi kuchangia kuzalisha ajira mpya milioni 8.

Imesema katika kufanikisha hilo itazifanyia mapitio sheria zote za biashara ili kuboresha zaidi mazingira ya kufanya biashara nchini na kuiwezesha sekta binafsi kuzalisha ajira na kuchangia kukua kwa uchumi na kuongeza pato la taifa.

Ahadi hiyo imetolewa jana na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaji, katika hafla ya kuwakabidhi zawadi za fedha taslimu Shilingi milioni 60, kwa washindi watatu wa kwanza wa shindano la ubunifu wa miradi kwa vijana wa kitanzania, iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Katibu Mkuu, Ali Gugu, Waziri Kijaji amesema, sekta binafsi ndio injini ya uchumi wa taifa, hivyo serikali ya awamu ya 6, itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili wajasiriamali wadogo na wakati nao wakue na kuzalisha kada ya mamilionea na mabilionea wazawa ambao watachangia katika uchumi wa taifa.

"Sisi kama serikali ya Mama Samia, neno letu kubwa tunalosema, na tunaloendelea kusema, tuweke mazingira mazuri ya biashara nchini, tunafanya kila jitihada kuhakikisha wawekezaji waliopo nchini, wanafanyabiashara zao na uwekezaji wao, katika hali ya utulivu bila kuwa na kero ya kodi korofi ambazo zinafifisha utendaji wao, lengo la kufanya hivi ni kuhakikisha wanaongeza uzalishaji kukidhi soko la ndani na ziada kuuza nje," alisema Gugu.

"Sisi serikali lengo letu kwa kuzingatia dira yetu ya 2025 ni kuzalisha ajira milioni 8, ili kutimiza lengo hili ni lazima kuishirikisha sekta binafsi, kwa serikali kuwajengea mazingira mazuri ya kufanya biashara kwa kuzalisha ajira mpya," alisema Gugu.

Aliipongeza Kampuni ya Mafuta ya TotalEnergies kwa shindano hilo, na kutoa zawadi za zaidi ya shilingi milioni 100, kati ya hizo, washindi watatu wa mwanzo, kila mmoja amepewa hundi ya shilingi 20 za Kitanzania kuboresha mitaji yao na kuwalea kwa mwaka mmoja kwa kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo na kuwaangazia fursa za masoko.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TotalEnergies Tanzania, Jean-Francois Schoepp, mesema lengo la kampuni ya TotalEnergies, kudhamini wabunifu hao ni ili kuwajengea uwezo Watanzania. "TotalEnergy, haifanyi tuu biashara na kuzalisha faida, bali kuitumia faida hiyo inayopatikana, kuwajengea uwezo na wengine ili kuwainua Watanzania na kuliinua taifa kiuchumi.

Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano, Getrude Mpangile, aliwataja washindi hao ni Costantine Edward wa kampuni ya AgriLife ambayo inatengeneza chakula cha mifugo kwa kuzalisha wadudu wanaotunza mazingira kwa kula uchafu na kuzalisha mbolea na chakula cha mifugo chenye viini lishe vingi.

Mwingine ni Innocent Sule wa kiwanda cha Soma Factories Tanzania Group ambao wanatengeneza mabegi ya shule yenye taa ya solar ya kusomea, kwa kutumia malighafi ya vitu vilivyotumiki ambavyo vingetupwa kama uchafu.

Wa tatu ni binti Hellena Sailas wa kampuni ya Arena Recycling Industry ambaye anazalisha matofali ya ujenzi kwa kutumia taka ngumu za plastiki, anazisaga na kutengeneza matofali ya ujenzi ambayo ni rafiki kwa mazingira na hayapitishi maji.

Mpangile amesema kilo mmoja amepatiwa fedha taslim, shilingi milioni 20 za Kitanzania kuboreshea mitaji yao, na watapatiwa mafunzo ya kulelewa kwa muda wa mwaka mmoja kuboresha biashara zao, na kupatiwa fursa ya kutangazwa na kufunguliwa fursa za masoko.

Watanzania 1,000 wameshiriki, kati ya hao, miradi 439 ndio ilikidhi vigezo, kati ya hiyo miradi 15 ikaingia fainali ndio wakapatikana hao washindi watatu. Shindano hilo la 'STARTUPPER OF THE YEAR CHALLENGE BY TOTAL-

# Polisi yazingira makao makuu NCCR-Mageuzi

**Na Jenipher Gilla**

POLISI wenye silaha jana walionekana kuzingira ofisi za Chama cha NCCR-Mageuzi zilizoko Mtaa wa Kilosa, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam, kutokana na vurugu zilizotokea baina ya wafuasi wa chama hicho.

Vurugu hizo ziliibuka baada ya Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi, kutangaza kumsimamisha Mwenyekiti wake, James Mbatia na Makamu Mwenyekiti Bara, Angelina Mtahiwa, hadi mkutano mkuu utakapoitishwa ili wajieleze kuhusiana na tuhuma zinazowakabili.

Baada ya kutangazwa kwa taarifa hiyo, Mbatia alisema hatambui mkutano uliofanyika wa Halmashauri Kuu kumsimamisha na kusisitiza kikao hicho ni batili.

Nipashe ilifika makao makuu ya ofisi hizo na kukuta gari la polisi likiwa na askari wenye sare na nguo za kiraia limeegeshwa Mtaa wa Kilosa, nyumba ya nne kutoka makao makuu ya chama hicho, wakilinda.

Kadhalika, ofisi hizo zilikuwa zimefungwa na hakukuwa na mtu yeyote aliyeruhusiwa kufika katika eneo hilo. Rajab Issa, mkazi jirani na ofisi hizo, alisema jana hakukuwa na vurugu, lakini polisi walikuwapo kwa ajili ya kulinda usalama tangu asubuhi. Alisema alishuhudia vurugu za wafuasi na viongozi wa chama hicho na polisi walifika na kuwadhibiti kwa kuwatawanya.

Jafari Mohamed, alisema migogoro ndani ya vyama haifurahishi akiwa kama kijana na kwamba wanaona siasa ni vurugu.

"Hainivutii kama kijana naona kuwa kiongozi wa siasa ni kuweka maisha yangu hatarini. Sipati amani kuona polisi wenye silaha wako kwenye mtaa wetu tunaona wakati wowote risasi zinaweza kupigwa na hapa kuna watoto wanacheza, sipati amani kuona polisi wamesimama hapa," alisema Said Lidenge.

Salim Zuberi mkazi wa eneo hilo, alisema migogoro ndani ya chama ndiyo inayojenga na kwamba kama jirani wa eneo hilo, hajashangazwa na kilichotokea ingawa hakupenda ifikie hatua ya watu kupigana.

Juzi, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania, Sisty Nyahoza, alisema ofisi yake ni mlezi wa vyama vya siasa vyenye usajili kamili na wanavilea kwa mujibu wa sheria na kwamba wanasubiri taarifa kamili kutoka NCCR-Mageuzi ndipo watatoa msimamo.

Alisema awali walipokea barua ya mabadiliko ya bodi ya wadhamini ambayo kulikuwa na ajenda ya kumsimamisha mwenyekiti.

**SAKATA ZIMA**

Baada ya kumalizika kwa Halmashauri Kuu, Katibu Mkuu wa NCCR-Mageuzi, Martha Chiambo, akiwa ameongozana na walinzi walifika makao makuu ya chama hicho na kuamuru ofisi hizo kufungwa. Baada ya katibu huyo kuondoka na kuacha vijana wakilinda eneo hilo, Katibu Mwenezi wa chama hicho, Edward Simbeye, alifika na kufungua ofisi hizo kisha kuzungumza na waandishi wa habari.

Alipomaliza, Mbatia aliwasili akiwa na Makamu Mwenyekiti Zanzibar na kuingia moja kwa moja ndani ya ofisi bila kuongea na mtu, na kundi lililokuwa limeachwa kulinda ofisi hizo lilimsogelea Mbatia akiingia ndani ndipo ugomvi upoibuka baina ya makundi hayo mawili.

# Mganga Mkuu asimamishwa kazi madai wizi wa mafuta

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro imemsimamisha kazi Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dustan Mshana, kwa tuhuma ya wizi wa mafuta lita 100, kununua kumpyuta chakavu pamoja na kutosimamia vizuri idara yake hiyo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Rachael Nyangasi, alisema hayo juzi kuwa mbali na huhuma hizo, pia Dk. Mshana anatuhumiwa kushindwa kusimamia mapato lindwa ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya ofisi yake.

"Dk. Mshana anatuhumiwa kufoji saini za madereva na kuchukua mafuta lita 100 za magari ya halmashauri hii, lakini ameshindwa kutii maagizo ya mwajiri wake yaliyomtaka kuwasilisha kumpyuta mpya na sio chakavu," alisema Nyangasi.

Nyangasi alisema mwajiri alimtaka Dk. Mshana kununua kompyuta 19 mpya kwa ajili ya kukusanya mapato lindwa, lakini katika ukaguzi uliofanywa na mkaguzi wa ndani umebainika kuwa ni kumpyuta tatu pekee ndiyo mpya na nyingine ni chakavu.

Alisema Baraza la Madiwani limeona itoe uamuzi huo wa kumsimamisha Mganga Mkuu huyo ili iwe fundisho kwa watumishi wengine wa wilaya hiyo ya Gairo wasiokuwa waadilifu na amewataka watumishi kuwa na waledi.

Mwenyekiti huyo alisema katika ununuzi wa kompyuta hizo kuna watumishi wengine kadhaa wanaotuhumiwa kuhusika na baraza limemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri kuchukua hatua stahiki kwa wahusika wote.

"Serikali imeongeza mishahara kwa watumishi wake, lakini bado kuna baadhi ya watumishi wasio waadilifu na kusababisha kutumia fedha zinatotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya wana Gairo kwa matumizi yao binafsi, hili halikubariki," alisema. Aidha, aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato kwenye kata zao na pia aliwahimiza kuhakikisha waziba mianya yote ya upotevu wa mapato kwa maslahi mapana ya maendeleo ya Gairo na taifa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabiri Makame, alisema wote waliohusika na hoja za Mkaguzi wa Fedha za Serikali (CAG), wachukuliwe hatua kali ili kitendo hicho kisiweze kujirudia tena upya katika wilaya yake hiyo.

Makame ametaka fedha zote za miradi ya maendeleo wilayani hapo zitumike vizuri na pia miradi ikimilike kwa wakati na pia alivitaka vikundi vyote vilivyochukua mikopo kuhakikisha vinarejesha mikopo hiyo kwa wakati.

Masatu Mdidi, Diwani wa Kata ya Kibedya, alisema wananchi wa Gairo wanashauku kubwa ya kupata maendeleo hivyo madiwani wote wana kila sababu ya kuhakikisha wanafanya kazi ipasavyo katika suala zima la ukusanyaji mapato.


**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO.........69.........OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE VENANCE JOSEPHAT KABULA DECEASES**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY JAPHET VENANCE KABULA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN NO 369 OF 1963)**

**All PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 Day of 6............2022
**Dated at Dodoma this 20..................day of 5..................... 2022**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MICHAEL WOLFRAM NGAIRO** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili T 779 ARW – ESCUDO SUZUKI. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa ya Polisi:**
**MBE/MBE/RB/194668/202**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KOROGWE**
**SHAURI LA MIRATHI NA.........2 YA 2022**
**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya**
**JOYCE MICHAEL MASHAKA.................MAREHEMU**
**DHIDI YA**
**JAMES HEBERT MASHAKA..................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**{Kanuni ya 75}**

Watu wote wanaodai kuwa na Haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu, wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 28 Mwezi wa 05 Mwaka 2022.
Hati hii imetolewa tarehe 13 Mwezi 05 Mwaka 2022.

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KOROGWE**



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO...........45........ 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BURTON AMULIKE MBOYA of Mkonze within Dodoma City**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY HOLLAND BURTON MBOYA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 OF 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 09.......... day of...........6............ 2022
Dated at Dodoma this 29............day of................ APRIL................ 2022

RESIDENT MAGISTRATE



STAR CITY




CONTACT US FOR PRICE





* 1st Phase 300 Acres for Commercial & Industrial Use
* Land is along the Dar to Mbeya Highway
* Within Morogoro city
* Flat Land
* Plots ranging from 0.5 to 5.5 Acres
* Individual Titles will be given
* Accessability to SGR

CONTACT US... +255 715 415 145 +255 783 278 787 - +255 783 124 688 - sales.starcitytz@gmail.com



Mkurugenzi Mtendaji wa MeTL Group, Mohamed Dewji Maarufu 'Mo', akitunukiwa udaktari wa heshima na Rais wa Chuo Kikuu cha George Town, John DeGiola (kulia), Marekani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaleta tozo mpya Kigamboni

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imefanya mabadiliko ya tozo za kuvuka katika Daraja la Kigamboni na kuweka utaratibu mpya wa kutoza safari kwa siku, wiki na mwezi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Fausine Ndugulile, kuanza kutumika kwa mfumo huo mpya ulioanza Mei 20 mwaka huu, tozo ya siku itamwezesha mtu kuvuka kwa idadi yoyote ya safari.

Alisema nauli za wiki na mwezi zitachelewa kuanza kutokana na kazi inayoendelea ya kuboresha mifumo, huku akibainisha gharama mpya zilizowekwa kwa upande wa bodaboda ambayo ni Sh. 300 kwa safari moja badala ya 600 ya awali, Sh. 500 kwa siku, Sh. 2000 kwa wiki na Sh. 5000 kwa mwezi.

Kwa upande wa Bajaji alisema zitalipa Sh. 500 kwa safari moja badala ya 1,500 ya awali, Sh. 3000 kwa siku, Sh. 10,000 wiki na Sh. 20,000 mwezi.

Aidha, magari Sh. 1,500 safari moja kutoka 5,000 ya awali, Sh. 2,500 kwa siku, Sh. 12,000 kwa wiki na Sh. 35,000 kwa mwezi.

"Kipekee namshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusikia kilio cha wana Kigamboni na kuagiza suala hili kufanyiwa kazi, Waziri Makame Mbarawa na Prof. Joyce Ndalichako kwa ushirikiano wao pomoja na makatibu wakuu Injinia Aisha Amour na Profesa Jamal Katundu kwa kulibeba jambo hili kwa uzito unaostahili na kulifanyia kazi.

"Namshukuru Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba na menejimenti yake kwa ushirikiano wao, na kilio cha wana Kigamboni ni kuondolewa kabisa tozo za daraja la Nyerere, natumai serikali itaendelea kulifanyia kazi suala hili," alisema Ndugulile.

Mmoja wa wananchi wa Kigamboni, Emmanuel Lyimo, aliliambia gazeti hili kwamba kilio chao kikubwa ni kutaka kufutiwa tozo za kupita katika daraja hilo huku akihoji sehemu zingine watu wanapita bila kulipa, lakini hapo wanalipa.

"Muda si mrefu nilipita pale wakasema suala la kulipia kwa mwezi halipo kwenye miongozo yao na endapo mtu atataka kulipa kwa utaratibu huo atapigiwa hesabu ya siku 30 kwa gharama ile ile ya 1,500," alisema Lyimo.

# Mwalimu Mkuu ahukumiwa jela miaka 3 kughushi fedha za ujenzi

**Na Samson Chacha,** TARIME

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Mwenge wilayani Rorya mkoani Mara, Issaya Gwidana, amehukumiwa kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya Shilingi milioni mbili baada ya kupatikana na hatia ya makosa sita ya kughushi nyaraka na hundi za shule na kujipatia Sh. 4,965,000.

Alisomewa hukumu hiyo mwishoni mwa wiki na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Tarime, Veronica Seleman.

Awali, Mwanasheria wa Serikali kitengo cha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mwinyi Yahaya, alidai kuwa mtuhumiwa ambaye ni mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Mwenge, alighushi nyaraka na hundi za shule hiyo na kujichukulia Sh. 4, 965,000 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule hiyo kinyume cha Sheria Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2019 na kuisababishia hasara serikali.

Hakimu alisema kuwa mahakama imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka bila ya

kuacha shaka yoyote na mshtakiwa anatiwa hatiani kwa makosa yote sita aliyoshtakiwa nayo ya kughushi nyaraka na hundi na kujipatia kiasi hicho cha fedha kilichokuwa kimeletwa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na kukwamisha juhudi za serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo.

"Nina mhukumu mtuhumiwa Issaya kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya Shilingi milioni mbili na kulipa fedha hizo za ujenzi wa madarasa alizochukua Sh. 4,965,000 ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye nia na tabia kama hii ya kujichukulia mali ya mwajiri wake bila kufuata utaratibu na kukwamisha miradi ya serikali," alisema Hakimu Veronica.

Mpaka mwandishi wa habari anatoka eneo la tukio mshtakiwa alikuwa hajalipa faini na kupelekwa gerezani.

# Mo Dewji atunukiwa PhD nchini Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA bilionea Mohammed Dewji maarufu MO, ametunukiwa udaktari wa falsafa (PhD) na Chuo Kikuu cha Georgetown McDonough School of Business cha Marekani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana kwenye tovuti ya chuo hicho kilichoko Washington D.C, Rais wa Chuo Kikuu cha Georgetown, John DeGioia ndiye aliyemtunuku MO Dewji PhD ya heshima Ijumaa iliyopita chuoni huko kutokana na mchango wake mkubwa kwa jamii ya Tanzania.

MO Dewji ambaye mbali na biashara, amewekeza kwenye michezo, ni Mkurugenzi Mtendaji wa MeTL Group na Mwasisi wa Taasisi ya Mo Dewji ambayo inatoa huduma za hisani ikiwamo katika sekta za elimu na afya.

MO Dewji alihitimu katika Chuo Kikuu hicho cha Georgetown McDonough School of Business mnamo mwaka 1998 na aliporejea nchini aliitumia elimu ya biashara aliyoipata huko na kuipa mafanikio makubwa MeTL Group.

"Tunampongeza na anastahili heshima hii," chuo hicho kilitamka kupitia taarifa hiyo iliyoambatanishwa na picha za MO Dewji akitunukiwa PhD na alipohutubia kwenye mahafali ya chuo hicho Ijumaa iliyopita.

Katika hotuba yake wakati wa mahafali hayo, MO Dewji aliwataka wahitimu na wanafunzi wanaoendelea na masomo chuoni huko, kuzingatia misingi ya biashara, akisema: "Dunia siyo yako, lakini siku zote inakuhusu".

MO Dewji alisisitiza umuhimu wa kutumia watu wanaokuzunguka, kujitolea kwa wengine na kujenga jamii iliyo imara.

Aliwataka wanafunzi 776 wanaoendelea na masomo na wahitimu 330 katika Shule ya Biashara ya McDonough ya chuo kikuu hicho kwa kukumbuka umuhimu wa kubadilishana mawazo kwa lengo la kuwajibika kwa jamii na kumjali kila mtu.

Pia aliwataka wanafunzi kutotoka nje ya misingi muhimu wanapoendelea na masomo yao, pia watakapokuwa wanatekeleza kwa vitendo walichokisomea.

"Sina shaka na yeyote kati yenu katika kuzingatia misingi hiyo," MO Dewji alisema na kutoa angalizo kwamba: Tambueni hili, kadri unavyofanikiwa, ndipo inapokuwa rahisi zaidi kwako kusahau namna unavyoihitaji jamii yako".

Katika orodha ya mwaka huu ya mabilionea duniani iliyotolewa na jarida maarufu la biashara la Forbes, Mo Dewji ameendelea kung'ara akiwa bilionea namba moja Tanzania na Afrika Mashariki, pia akiingia kwenye orodha ya mabilionea barani Afrika.

Kwa mujibu wa Forbes, Mo Dewji kwa sasa anashika nafasi ya 15 kwenye orodha ya mabilionea barani Afrika akiwa na utajiri unaofikia Dola za Marekani bilioni 1.5.

TANGAZO



# Tumefungua Maombi ya Ufadhili wa Masomo na Mafunzo kwa Ushauri ya NMB Nuru Yangu kwa Mwaka 2022

Kwa Wanafunzi wanaoingia Kidato cha Tano na Elimu ya Juu

NMB FOUNDATION

## KUHUSU UFADHILI HUU

NMB Foundation imeanzisha mpango wa ufadhili wa masomo na mafunzo kwa ushauri kupitia program ya Nuru Yangu, yenye lengo la kuunga mkono sekta ya elimu, kupunguza umaskini na kuendeleza kizazi kijacho cha viongozi, kwa kuongeza wigo wa upatikanaji wa elimu ya sekondari na vyuo vikuu.

Tunatazamia kuchochea uwezo wa vijana wenye kiu ya maarifa, wanaotazamia kesho iliyo bora na wenye shauku ya kuleta mabadiliko ulimwenguni. Huu ni mpango wa masomo na ushauri unaolenga kuwanufaisha vijana wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini wenye uwezo mzuri kimasomo na walio na bidii zenye kuleta matokeo chanya kwa maendeleo ya jamii yetu.

## Kidato cha Tano

Waombaji watakaofanikiwa watapatiwa ufadhili kamili, ambao utahusisha gharama zote za moja kwa moja zinazolipwa shuleni ikiwemo ada ya masomo, uniform ,vitabu ,madaftari ,nauli za kwenda na kurudi kwa walio kwenye shule za bweni, hela ya kujikimu (pale inapohitajika), pamoja na kadi ya matibabu ya NHIF na mahitaji mengine kama yalivyooanishwa kwenye fomu ya kujiunga na shule.

### VIGEZO VYA USTAHIKI

Ili kukidhi vigezo kwa ajili ya mpango wa **ufadhili wa masomo na programu ya ushauri ya Nuru Yangu** *(Nuru Yangu Scholarship and Mentorship Program)*, waombaji wote lazima wakidhi vigezo vyote vya ustahiki hapo chini:

1. Lazima uwe raia wa Tanzania ambaye umemaliza kidato cha nne mwaka 2021.
2. Uwe na matokeo bora katika mitihani ya kidato cha nne, (divisheni 1 point 7-14).
3. Lazima uwe umechaguliwa katika moja ya shule za umma, kwa masomo ya kidato cha tano 2022.
4. Lazima kuonyesha uhitaji wa kifedha.

**Nyaraka zinazohitajika kuambatanishwa na maombi;**

1. Barua ya maombi ikielezea kwanini upewe ufadhili
2. Barua ya udhamini kutoka ofisi ya Mtendaji Kata.
3. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
4. Nakala ya Cheti cha kifo (kama umefiwa na mzazi mmoja au wote).

### UTARATIBU WA MAOMBI

Tumefungua maombi ya ufadhili wa masomo na ushauri wa Nuru Yangu kwa mwaka wa masomo unaowahusu wanafunzi wanaoingia kidato cha tano mwaka 2022. Waombaji wote, ambao wanakidhi vigezo wanahimizwa kuomba kwa kujaza fomu inayopatikana kupitia **www.foundation.nmbbank.co.tz** au kwenye **tawi lolote la benki ya NMB**.

**Mwisho wa Kujisajili ni :**
**10 Juni 2022, 10:00jioni.**

## Elimu ya juu

Waombaji watakaofanikiwa watapatiwa ufadhili kamili, ambao utahusisha gharama zote za moja kwa moja zinazolipwa chuoni ikiwemo ada ya masomo, pamoja na gharama za mwanafunzi (chakula, malazi, vitabu na vifaa, mafunzo kwa vitendo na mahitaji muhimu ya kitivo) kama ilivyoainishwa katika muongozo wa gharama wa chuo. Mfadhiliwa pia atapatiwa kompyuta mpakato na mshauri atakaemsaidia kukua katika taaluma yake.

### MASOMO HUSIKA

Mpango huu wa ufadhili unalenga **kufadhili wanafunzi 50** kwa shahada za chuo za masomo mbalimbali yakiwemo:

- Business
- Oil and Gas
- Medicine
- Engineering
- Actuarial Science
- Computer Science or ICT
- Mathematics and Statistics
- Finance and Commerce
- Economics
- Data Science
- Data Mining
- Risk Management

** Masomo ambayo hayapo katika orodha iliyotajwa hapo juu, yatapata idhini kulingana na maamuzi ya NMB Foundation.*

### VIGEZO VYA USTAHIKI

Ili kukidhi vigezo kwa ajili ya mpango wa **ufadhili wa masomo na programu ya ushauri ya Nuru Yangu** (Nuru Yangu Scholarship and Mentorship Program), waombaji wote lazima wafikie vigezo vyote vya ustahiki hapo chini:

1. Lazima uwe raia wa Tanzania ambaye amemaliza Shule ya Sekondari (Kidato cha Sita).
2. Uwe na matokeo bora katika mitihani ya Kidato cha Sita Advanced Certificate of Secondary Education Examinations (ACSEE) divisheni 1 pointi 3-7.
3. Ufaulu mzuri katika matokeo ya kidato cha nne, divisheni 1 point 7-14 ni sifa ya nyongeza.
4. Lazima uwe na umri chini ya miaka 30.
5. Lazima uwe umechaguliwa katika moja ya chuo kikuu cha umma au taasisi ya juu ya umma inayotambulika, kwa masomo ya muda wote kwenye moja ya kozi zilizoainishwa kuwa sehemu ya program ya Nuru Yangu.
6. Lazima kuonyesha uhitaji wa kifedha.

**Nyakara zinazohitajika kuambatanishwa na maombi (zote ziwe zimehakikiwa)**

1. Nakala ya majibu au vyeti vya NECTA vya sekondari kidato cha nne na cha sita.
2. Nakala ya Cheti cha kifo (kama umefiwa na mzazi mmoja au wote).
3. Ushahidi/uthibitisho (kama umeonyesha kuwa na mahitaji maalumu katika fomu ya maombi)
4. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
5. Barua ya udhamini kutoka ofisi ya Mtendaji Kata.

### UTARATIBU WA MAOMBI

Tumefungua maombi ya ufadhili wa masomo na ushauri ya Nuru Yangu kwa mwaka wa masomo 2022/2023. Waombaji wote, ambao wanakidhi vigezo wanahimizwa kuomba kwa kujaza fomu inayopatikana kupitia **www.foundation.nmbbank.co.tz**

ANGALIZO 1: Hakikisha UNASOMA maagizo YOTE na unaelewa kabla ya kutuma maombi.

ANGALIZO 2: Hakikisha unajaza fomu ya maombi na kuikabidhi kwenye tawi la benki ya NMB lililokaribu na makazi yako. (kwa maombi ya kidato cha tano).

ANGALIZO 3: Hakikisha nyaraka zote zinazohitajika zinaambatanishwa na maombi yako yakiwa na taarifa sahihi, maombi yatakayokuwa na udanganyifu yataondolewa kwenye mchakato.

ANGALIZO 4: Sambamba na uombaji wa ufadhili wa programu ya chuo kikuu waombaji wanaimizwa kufanya maombi ya ufadhili wa Bodi ya Mikopo (HESLB). Hata hivyo, endapo muombaji atapata ufadhili wa program ya Nuru Yangu na HESLB, atatakiwa kujitoa kwenye udhamini wa HESLB pindi tu wapatapo ufadhili huu.

ANGALIZO 5: Waombaji wote wanaokidhi vigezo vilivyotajwa wana fursa sawa.

**Mwisho wa Kujisajili ni:**
**30 Septemba 2022, 10:00jioni.**

Elimu

**Kwa taarifa zaidi kuhusu maombi ya Nuru Yangu Scholarship and Mentorship Program:**
**Tutumie barua pepe: foundation@nmbbank.co.tz** au
**Tupigie kupitia namba: 0800 002 002**

***foundation.nmbbank.co.tz***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF tunataka waamuzi bora 'dabi' Simba, Yanga Kirumba

**MIAMBA** ya soka nchini, Simba na Yanga zitashuka tena dimbani Jumamosi wiki hii, safari hii zikivaana kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu FA Cup.

Timu hizo zitamenyana katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza ikiwa ni mara ya tatu msimu huu baada ya kukutana mara mbili kwenye Ligi Kuu na kutoka sare tasa, lakini pia hiyo inaweza kuwa mara ya nne kama itajumuishwa na mechi ya Ngao ya Jamii maalum kwa ajili ya kufungua msimu wa 2021/22, ambao Yanga ilishinda bao 1-0.

Simba itashuka dimbani hapo ikitoka kuvaana na Geita Gold jana katika uwanja huo wa CCM Kirumba kwenye mechi ya Ligi Kuu, lakini Yanga leo itavaana na Biashara United uwanjani hapo kwenye mechi nyingine ya ligi hiyo kabla ya Jumamosi miamba hiyo kukutana.

Kwa ujumla ni mechi ambayo tayari imeanza kuvuta hisia za mashabiki na viongozi wa klabu hizo kwa kila mmoja kutamba ataibuka na ushindi katika mchezo huo ambao ni safari ya kuwania tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho Afrika.

Wakati Simba ikitamba itawashushia wapinzani wao hao 'pumzi ya moto', Yanga wamesema siku hiyo itabidi watani wao hao wa jadi wawaeleze ni namna gani walipata sare mbili katika mechi za Ligi Kuu dhidi yao msimu huu, hizo zikiwa ni baadhi ya tambo ambazo zinaendelea kuchagiza na kuvuta hisia za mchezo huo.

Ikumbukwe pia, mshindi wa mechi hiyo atakutana fainali na timu itakayoshinda katika nusu fainali ya pili itakayopigwa kesho katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha kati ya Azam FC na Coastal Union ya Tanga ili kuwania tiketi hiyo ya kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Hata hivyo, pamoja na yote hayo sisi tunataka kuona mchezo wa kiungwana zaidi ukitawala kuanzia uwanjani kwa wachezaji, waamuzi, mabenchi ya ufundi hadi kwa viongozi wa klabu hizo kongwe zaidi nchini.

Hatutarajii kuona waamuzi wa mchezo huo wakiegemea upande wote ama mashabiki wakikosa staha katika ushangiliaji wao, kwa kuwa matarajio yetu ni kushuhudia sheria 17 za soka zikitekelezwa ipasavyo na mashabiki wakishangilia mwanzo mwisho pasipo madhara kwa yoyote.

Tunatambua Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 63 huku Simba ikiwa nyuma yake kwa tofauti ya pointi 13 (kabla ya mchezo wake wa jana), timu hizo zote zinanafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu ujao hata kama zisingesonga mbele katika michuano hiyo ya FA Cup.

Lakini hilo haliwezi kuondoa ushindani katika mchezo huo kwani matokeo yoyote miamba hiyo inapokutana, huingia kwenye rekodi, huku pia wakati Yanga ikihitaji kushinda ili kuwa katika mbio ya kunyakua mataji yote mawili kama ilivyofanya Simba msimu uliopita, watani wao hao nao wanataka angalau kumaliza na taji moja msimu huu.

Kwa mantiki hiyo, haitakuwa mechi ya kusaka heshima pekee, bali ushindi na rekodi ambayo itaendelea kudumu vinywani vya mashabiki wa soka ndani na nje ya nchi, hivyo waamuzi hawana budi kuitenda haki kwa kufuata sheria zote 17 za soka ili mshindi awe aliyestahili.

Aidha, huu ni wakati sasa kwa klabu hizo kuendelea kufanya maandalizi ya kutosha ili Jumamosi mashabiki wa soka wapate burudani waliyoitarajia na kutojutia fedha zao watakazotoa kwa ajili ya kushuhudia mchezo huo.

Tunatarajia kuona Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kushirikiana na kamati zake za Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), zikituletea waamuzi bora na wazoefu wa mechi kubwa hususan za watani hao wa jadi nchini, ili Watanzania waifurahie dabi hiyo ya funga msimu nchini.

Pamoja na hayo pia tunatamani kuona Jumamosi mashabiki wakijitokeza kwa wingi zaidi ili kuujaza Uwanja wa CCM Kirumba, jambo ambalo litatoa hamasa kwa wachezaji wa kila timu kufanya vizuri, lakini wataliongezea hadhi dabi hilo la soka nchini ambalo huvuta hisia za wapenzi wa soka hadi nje ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Ihefu, DTB kupanda Ligi Kuu, jipangeni mapema

Na Adam Fungamwango

**IHEFU** na DTB ni moja kati ya timu zitakazocheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2022/23, baada ya kupanda zikitokea Ligi ya Championship.

Ligi ya Championship, ilimalizika juzi na timu hizo kupanda, hivyo kukata tiketi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao, baada ya zote mbili kumaliza zikiwa na pointi 66.

Ihefu, ndiyo imekuwa bingwa wa Ligi ya Championship kwa kuizidi DTB mabao, kwani imemaliza ikiwa na mabao 50, huku DTB wakiwa na mabao 44.

Timu hizi zimeingia Ligi Kuu zikiwa na rekodi zinazotofautiana. DTB ni timu mpya na ndiyo mara ya kwanza kabisa kupanda. Hata hivyo, ina wachezaji ambao hawatokuwa mara ya kwanza kucheza Ligi Kuu. Huenda baadhi wanaweza kuondoka na kwenda kwenye klabu zingine. Nina uhakika wengine wengi watabaki kutokana na kuwa klabu hiyo inaonekana kujiweza kifedha.

Pia inaweza kusajili wachezaji wengine kutoka timu mbalimbali za Ligi Kuu.

Baadhi ya wachezaji waliotoa mchango mkubwa kuipandisha DTB ni Amissi Tambwe, Mrundi aliyewahi kuzichezea klabu za Simba na Yanga ambaye ameifungia mabao 14, Tafazwa Kutinyu raia wa Zimbabwe, alikipiga na timu za Singida United na Azam FC, James Kotei na Nicolaus Gyan aliyemaliza na mabao 12, Waghana ambao waliichezea klabu ya Simba, Juma Abdul nahodha wa zamani wa Yanga na wengineo wengi.

Hii ina maana pamoja na kwamba DTB itakuwa timu ngeni, lakini itakuwa ni jina tu, wachezaji watakuwa ni wale wale wazoefu kwenye Ligi Kuu. Inawezekana ikawa moja ya timu hatari na tishio.

Ihefu ambao ndiyo mabingwa wapya, si timu ngeni kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Haikuwapo kwenye msimu huu tu unaomalizika.

Msimu uliopita 2020/21 ilicheza Ligi Kuu, lakini ikaporomoka. Na ilipanda na kucheza na msimu mmoja tu kabla ya kushuka.

Nadhani sasa viongozi wa klabu hiyo watakuwa wanajua sababu ambazo zilifanya timu ishike, hivyo wanatakiwa wazitafutie dawa ili yasiwakute tena yaliyowakuta.

Viongozi wa timu zote mbili watakuwa wanaiona Ligi Kuu Tanzania Bara jinsi inavyoishia na timu nyingi zikiwa kwenye janga la kushuka daraja.

Watakuwa wameshapata somo ni kwa sababu timu nyingi pointi zao zimekaribiana sana.

Wanachotakiwa kufanya ni kutafuta wachezaji ambao uwezo wao ni mkubwa zaidi kuliko hawa waliopo kwenye Ligi Kuu.

Sisemi kwamba wasisajili wachezaji waliopo kwenye Ligi Kuu, la hasha, ila inavyoonekana ni kwamba timu nyingi za Ligi Kuu wachezaji wao viwango vinafanana sana, labda ukiondoa Simba, Yanga na kidogo Azam.

Ndiyo maana utaona hakuna tofauti kati ya Biashara United, Mtibwa Sugar, Dodoma Jiji, KMC, Polisi Tanzania, kwa sababu wachezaji mara nyingi ni wale wale tu wanaozunguka kila msimu kutoka klabu hii kwenda nyingine.

Kama zinataka kuendelea kula matunda ya Ligi Kuu na si msimu mmoja tu zinashuka, basi ni kuwekeza kwa wachezaji bora na wa viwango vya juu.

Mfano Yanga, imesajili wachezaji wenye viwango vya juu ndani na nje ya nchi ambao wanawapa matokeo.

Simba, pamoja na kwamba wachezaji wake wengi viwango vyao vimeporomoka, lakini bado haijafikiwa na timu zingine za chini na kabla ya mechi ya jana dhidi ya Geita Gold ilikuwa imeipita Azam FC, timu inayoshika nafasi ya tatu kwa pointi 14.

Kwa maana hiyo, DTB na Ihefu zinatakiwa kusajili wachezaji wenye viwango angalau kuzidi timu za kati kwenye msimamo wa ligi, ili ziwe salama msimu ujao.

Sina shaka sana na DTB kutokana na viwango vya wachezaji wao, ila wanatakiwa pia waongeze wengine, lakini Ihefu inatakiwa iwe makini kwa hilo, na si kuendelea kuwatumia wachezaji wengi waliopanda nao. Wanatakiwa wachanganye. Wawasajili pia na baadhi ya wachezaji wa Ligi Kuu wenye uwezo. Pia waondoke na kusaka wachezaji wengine wapya kutoka mataifa hata ya jirani ili kuipa nguvu timu yao.

Haipendezi kuona timu inapanda msimu huu na msimu huo huo mwishoni inashuka daraja, hongereni, ila jipangeni pia kwa kuwekeza kwa wachezaji na benchi la ufundi.

# SHIVYAWATA yataka utekelezaji sheria wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), limeiomba serikali kusimamia utekelezaji wa sheria ya watu wenye ulemavu kwa vitendo ili wapate haki ikiwamo ajira kama walivyo wengine kwenye jamii.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Wakili wa SHIVYAWATA, Novath Lukwago, wakati akiwasilisha mada ya sheria ya watu wenye ulemavu kwa wahariri wa vyombo vya habari nchini.

Alisema sheria ya ajira inamtaka kila mwajiri kuhakikisha anaajiri watu wenye ulemavu kwa asilimia mbili kati ya waajiriwa aliona, lakini kiuhalisia haiko hivyo na hakuna ufuatiliaji wowote.

Pia alisema sheria ya matunzo inataka serikali na jamii kutoa matunzo kwa wenye ulemavu ikiwamo matibabu, na kwamba Sheria ya Wenye Ulemavu ya 2010 ilianzisha rejista itakayowezesha ufuatiliaji wa ajira na wengi waliajiriwa.

Alisema katika sheria hiyo kamishna wa ajira alikuwa na mamlaka wakati wowote kuingia sehemu yoyote ya kazi na kuhoji utekelezaji wa ajira kwa kundi hilo.Alisema sheria imeweka usawa na kuondoa ubaguzi, ikiwamo mkakati wa kukabili ubaguzi na tishio lolote la usalama wa watu wenye ulemavu.

Kwa mujibu wa Lukwago, bado changamoto ni kubwa kwa kuwa waajiri hawana uelewa wa kutosha kwa kuwa wengi wana hofu ya hisia kumwajiri mwenye ulemavu licha ya kwamba ana sifa zote stahiki.

Alisema kikwazo kikubwa ni kuwa hakuna usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa kipengele cha ajira, kukosekana mkakati wa wizara inayohusika na ajira juu ya namna gani wataifikia asilimia tatu iliyowekwa kisheria.

"Kutokutekelezwa kwa takwa la kisheria la utaratibu wa kukusanya na kutoa taarifa ya hali ya ajira kwa watu wenye ulemavu kila mwaka. Mifumo ya ajira haijawa jumuishi kwa watu wenye ulemavu (kutangaza, kusaili na sehemu za ajira)," alisema.

Alisema ni muhimu serikali ikatoa motisha kwa waajiri wanaoajiri watu wenye ulemavu, ikiwamo kuwaondolea baadhi ya kodi, kwa kuwa wanaingia gharama zaidi kuweka miundombinu wezeshi na mazingira jumuishi.

Awali, akifungua mkutano huo Katibu wa SHIVYAWATA, Jonas lubago, aliviomba vyombo vya habari kuendelea kupaza sauti kwenye masuala ya watu wenye ulemavu ili jamii iwe na uelewa.

"Tunaona ahadi ni nyingi kwamba hiki na kile kitafanyika au kimeshafanyika lakini ukifuatilia utekelezaji wake bado ni mdogo au haupo kabisa. Tunaiomba serikali itekeleze sheria hii kwa ukamilifu wake, wengi licha ya kuwa wasomo wazuri ila ulemavu wao umewakosesha haki ya kuajiriwa," alisema.

Alisema ndani ya serikali, taasisi, mashirika na sekta binafsi wapo waajiri ambao hawajaajiri na huwakataa wenye ulemavu kwasababu wanaona ni gharama na kwamba wengi wamesoma wako mtaani wanahangaika.



Mkurugenzi wa Dijitali na Huduma za Ziada wa Vodacom Tanzania Plc, Nguvu Kamando (aliyevaa suti), akizungumza na mawakala wa kampuni hiyo walioko Tivoli jijini Mwanza, wakati watendaji wakuu wa kampuni hiyo walipowatembelea watoa huduma wao ili kusikiliza kero zinazowakuta na kujua hali halisi ya soko ilivyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watoto 256,186 wachanjwa polio

**Na Juliet Mkileri,** KIBAHA

WATOTO 256,186 wenye umri chini ya miaka mitano sawa na asilimia 127 wa Mkoa wa Pwani wamepatiwa chanjo ya polio.

Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Pwani, Abas Hincha, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu.

Hincha alisema katika siku nne za utoaji wa chanjo hiyo watoto hao wamefikiwa wakiwa nyumbani, shuleni na kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema baada ya siku za kampeni kukamilika vituo ambavyo malengo ya kutoa chanjo bado yapo chini vitaendelea na zoezi la kutoa chanzo.

Katika kampeni hiyo ambayo ilianza Mei 18 Mkoa wa Pwani ulitarajia kutoa chanjo ya matone ya polio kwa watoto zaidi ya 200,967, wenye umri chini ya miaka mitano.

Akizindua kampeni ya utoaji wa chanjo hiyo Mkuu wa Mkoa huo, Abubakar Kunenge, alisema lengo ni kuongeza kinga, kuzuia mlipuko na kudhibiti watoto wasipatwe na virusi vya polio ambao moja ya madhara yake ni ulemavu wa ghafla wa viungo.

Kunenge alisema sambamba na kampeni hiyo pia shughuli za ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za wagonjwa wote wanaopata ulemavu wa ghafla zitafanyika.

# Wataka mifumo kukabili ukatili wa kijinsia

**Na Jenifer Gilla**

VYOMBO vya habari vimetakiwa viwe na mifumo inayofanyakazi kumwezesha mwandishi wa habari kutoa taarifa anapopitia unyanyasaji wa kijinsia ili kumaliza tatizo hilo.

Hayo yalisemwa na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Habari - MAELEZO, Rodney Thadeus, hivi karibuni jijini Dar es Salaam, katika mkutano wa kisera na jinsia kwenye vyombo vya habari ulioandaliwa na Internews.

Rodney alisema moja ya mifumo hiyo ni kuwapo kwa kanuni inayomwonyesha mwandishi wa habari na mhariri misingi na kanuni za nafasi yake ili ajue mipaka yake awapo kazini.

"Ni muhimu kukumbusha vyombo vya habari kuweka misingi inayomwonyesha mwandishi wa haxqbari mipaka yake ya kazi, ili isiwe dhambi mtu kuingia kwenye uhusiano, lakini isiwe ya kulazimishwa," alisema Rodney.

Alisema serikali imeliona tatizo hilo na ipo tayari kushirikiana na vyombo vya habari kulitatua kwa njia mbalimbali, ikiwamo kutoa msaada wa elimu yaa sheria zinazohusu unyanyasaji mahali pa kazi, wajiri na waajiriwa wazielewe ili mfanyakazi anapopitia changamoto hiyo atoe taarifa.

"Panapotokea jambo linalokwaza au kurudisha nyuma tasnia ya habari taarifa zitolewe kwa habari maelezo na serikali, kwa usiri na kuchukua hatua stahiki," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Internews Tanzania, Angela Nicoara, alisema kuwa utafiti walioufanya unaonyesha kuwa wanawake wengi wanasoma masomo ya uandishi wa habari, lakini ni asilimia 40 ndiyo wanaofanya kazi hiyo.

"Taarifa mbaya ni kuwa waaandishi wa habari wengi wanaishia kufanya kazi katika ngazi za chini kutokana na changamoto nyingi kuwazuia kufikia nafasi za juu. Changamoto kubwa ni unyanyasaji wa kijinsia. Kwa ufupi unyanyasaji wa kijinsia umeshamiri katika vyombo vya habari na taaluma ya uandishi," alisema Angela.

Akiwasilisha matokeo ya utafiti waliofanya kuhusu unyanyasaji wa kijinsia katika vyombo vya habari, Mkurugenzi, Usawa wa Jinsia na Ushirikishwaji wa Jamii kutoka Shirika la Kimataifa la Kuboresha Afya na Ustawi wa Jamii (FHI 360), Andrea Bertone, alisema mfumo wa vyombo vya habari unawaacha wanawake na vijana nyuma hasa katika maendeleo ya kidigitali.

"Ili mwanamke aweze kwenda na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia katika vyombo vya habari inamlazimu kuwa na ujuzi mkubwa kwa suala hilo tofauti na mwanamume," alisema Andrea.

Alisema utafiti huo ulionyesha kuwa wanawake waandishi wa habari nchini, wanafanya kazi kwa bidii na hii yote ni kuwaonyesha wanaume uwezo wao ili kupambania nafasi za usawa.

Vilevile, alisema kuwa kuna mabadiliko katika uandishi wa habari za watu wenye ulemavu ingawa bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuongeza kasi huku akitolea mfano wa gazeti la Nipashe kuwa mfano bora wa uandishi wa habari hizo kwa kuziripoti kila siku.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, alisema elimu kuhusu masuala ya unyanyasaji wa kijinsia katika vyombo vya habari iwafikie pia wanaume kwa sababu nao wanahusika katika ukatili huo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TAWLA, Tite Mwabilile, alisema mila na desturi zinachangia kuwapo kwa unyanyasaji wa kijinsia kazini kwa kuwa jamii inaamini kuwa mwanamke hawezi kushika nafasi za juu na pia ni chombo cha kutolea maneno machafu.

Akitoa mada katika mkutano huo, Msanifu Mkuu Mkuu wa Kurasa kutoka Gazeti la Uhuru, Jane Mihanji, alisema kuwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vinajitokeza sio tu kwenye vyombo vya habari bali hata maeneo mengine ya kazi ikiwamo vitengo vya matangazo.

"Hata watu wanaohusika na matangazo wamekuwa wakilalamika kufanyiwa vitendo hivyo wanapokwenda kutafuta habari, na hujikuta kuingia kwenye mtego huo kulingana na mazingira na uhitaji wa matangazo hayo ili wapate commission," alisema.

Alisema njia ya kuondoa tatizo hili ni viongozi katika vyumba vya habari kukubali kuwa tatizo hili lipo, wawe wasikilizaji wa tatizo na kuchukulia hatua, kuwa makini na kujua ukweli ili kutatua tatizo.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN), Salome Kitomari, alisema ni muhimu kuwajengea uwezo wa kujiamini mabinti na wanawake wanaoingia kwenye taaluma hiyo.

"Tunapoona mwanamke anapitia unyanyasaji wa kijinsia halafu anakaa kimya inawezekana ilianzia katika ngazi ya familia, kwa hiyo anaishi na adabu ile ile ya kuvumilia ukatili, kumbe unaweza ukatoa taarifa suala hilo katika idara ya kazi," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela akiwasilisha ripoti yake katika Mkutano Mkuu wa 27 wa Wanahisa wa benki hiyo uliofanyika siku ya jumamosi tarehe 21/05/2022 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) na kupitia mtandao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waunga mkono Royal Tour kwa kusafisha mazingira

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kutangaza utalii wa nchi, wadau wa mazingira nchini wameanzisha kampeni ya siku 30 ya kusafisha fukwe za jijini Dar es Salaam ili ziwe rafiki kwa shughuli hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya kufanya usafi katika fukwe za Rainbow jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Asasi ya Kiraia ya Sustainable Development Network, Fredy Kwezi, alisema walivutiwa kufanya usafi katika eneo hilo baada ya kuona hali yake sio rafiki kwa utalii.

"Kwa hali tulioikuta hapa tumeona kuwa mtalii hawezi kuvutiwa kukaa hata kuogelea kutokana na uchafu wa aina mbalimbali kuzagaa pembezoni mwa bahari, sasa tukafikiria hatutokuwa tumeitendea haki juhudi ya rais ya kutafuta watalii kama kutakuwa na mazingira ya aina hii," alisema.

Aliiongeza kuwa kampeni hiyo itahusisha maeneo mengine ya fukwe mpaka pale watakapojiridhisha na hali ya usafi wa fukwe hizo.

Alisema usafi huo unaambatana na kutoa vifaa vya kuhifadhia taka pamoja na mabango ya kuelimisha jamii kuhusu utunzaji wa mazingira maeneo hayo na kutengeneza umoja wa wakazi wa eneo hilo ili kuhakikisha mazingira hayo yanakuwa safi muda wote

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Human Dignity and Environmental Care (HUDEFO), Sara Pima, alisema uchafu uliozagaa katika fukwe hizo sio tu rafiki kwa utalii bali hata afya ya Watanzania wenyewe ambao hutembelea karibuni kila siku.

"Tulikuja hapa siku ya sikukuu ya Idd tukakuta watoto wanaogelea katikati ya takataka kwa sababu hawawezi kuogelea kwenye maji mengi, hali ambayo inaweza kuwasababishia kupata maradhi ya ngozi hata kuhatarisha usalama wao kama ikitokea amekunywa maji kwa bahati mbaya," alisema Sara.

Ofisa uhifadhi wanyama kutoka kampuni ya utalii ya Tanzania Explorer, Veronica Donald, alisema wakiwa kama wadau wa utalii wameunga mkono kampeni na kushiriki kufanya usafi katika fukwe hizo ili wageni watakaowapokea watembelee maeneo ambayo ni masafi.

"Tunaamini Royal Tour itatuletea watalii wengi, hivyo tunasafisha fukwe hizi ili tupate eneo zuri la kuwaleta watalii, hapo mwazo tulikuwa hatuwaleti hapa kwa sababu wanakosa sehemu ya kuogelea na kupumzika kutokana na uchafu kuzagaa na kutoa harufu," alisema Caroline.

Mjumbe wa Mtaa wa Mbezi Beach na Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya mtaa huo, Caroline Ngoda, alishukuru wadau hao na kusema kuwa bado kazi inahitajika kuhakikisha kuwa mazingira ya eneo hilo yanakuwa mazuri kwa sababu hali ya fukwe hizo sio nzuri.

"Tunahitaji ushirikiano wa wadau kama hawa ili kuweka eneo hili safi kwa sababu kama unavyoona takataka hizi zinasababishwa na Mto Mbezi ambao ndio unaleta taka kutoka maeneo mengine ikiwamo Kimara, Mbezi kwa hiyo ni zoezi endelevu," alisema.

Naye mdau wa mazingira, Mhandisi Boniface Kyaruzi, alisema kuwa kutoa taka hizo hakutomaliza tatizo kama watu hawajabadilishwa mitazamo juu ya umuhimu wa kutunza fukwe hizo.

"Kama mindset za watu hazijabadilishwa hata hizi taka zikitolewa haitosaidia kitu, watu wanatakiwa wawe tayari kutunza mazingira ili tutakapoyaondoa haya yasirudi tena" alisema injinia. Tulishawahi kuja hapa tukakusanya taka zote hizi zikaisha lakini baada ya muda zikarudi.

Naye mmoja wa wafanyabiashara wa fukwe hizo Joyce Masawe alisema uchafu uliotatanda katika fukwe hizo unasababisha watalii kutotembelea eneo hilo hali inayofanya mauzo yao kuwa hafifu.

"Nipo hapa mwaka wa nane sasa napika chakula kwa ajili ya wahudumia watalii na watanzania wanaokuja kutembea, sio siri kadili siku zinavyokwenda watalii wanaotembelea eneo hili wanapungua kutokana na taka zilizozagaa pembezoni mwa bahari ambazo wakati mwingine zinatoa harufu,"alisema Joyce.

Alisema mbali na uchafu huo kuletwa na Mto Msimbazi lakini pia wakazi wa eneo hilo ambao hutupa taka nyakati za usiku ili wasionekane.

"Kuna watu wanakuja na matoroli wanakuja kumwaga taka pembezoni mwa bahari, nilijaribu kukemea wala hawakujali, tena wengine wanapewa taka za hospitalini na kuja kuzimwaga huku bila ya kujali athari zake kwa wenzao, tunaiomba serikali itusaidie kudhibiti watu hawa," alisema.

Jumla ya viroba 35 vya taka za plastiki vilikusanywa kukiwamo na chupa na plastiki na pamoja na taka hatarishi ikiwamo mabomba ya sindano.

## Wanahisa CRDB wapitisha gawio la hisa la Sh.36

**Na Maulid Mmbaga**

WANAHISA wa Benki ya CRDB wamepitisha mapendekezo ya bodi ya wakurugenzi kuhusu malipo ya gawio la Sh. 36 kwa kila hisa ambayo yanaleta jumla ya thamani ya gawio la mwaka wa fedha 2021/2022 kufikia Sh. bilioni 94.

Akizungumza katika mkutano mkuu wa 27 wa CRDB uliofanyika jana jijini Arusha, Mwenyekiti wa Bodi ya Benki hiyo, Dk. Ally Laay, alisema gawio hilo ni ongezeko la asilimia 64 ikilinganishwa na Sh. 22 kwa kila hisa iliyotolewa mwaka jana.

Alisema hiyo inaashiria ukuaji wa mapato kwa kila hisa ambapo katika kipindi cha mwaka 2021 yalikuwa Sh. 102.7.

"Kwa mara nyingine tena, tunafuraha kuwasilisha thamani endelevu kwa wanahisa wetu, utendaji wa benki katika mwaka wa 2021 ulitoa matokeo mazuri ambayo yanadhihirisha mafanikio ya mikakati yetu ya biashara, benki ilipata faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 268.2 ikiwa ni ongezeko la asilimia 62.3," alisema Dk. Laay.

Pia alibainisha kuwa kampuni tanzu za benki hiyo ziliendelea kuchangia vyema katika biashara ya kundi huku kampuni ya Burundi pekee ikichangia faida ya jumla ya Sh. bilioni 12.8 na ya bima Sh. milioni 859.0.

Aliongeza kuwa wamepata maendeleo makubwa katika kupata leseni na vibali vinavyohitajika kutoka kwa mamlaka za nyumbani pamoja na mataifa mengine, huku wakitarajia kuanza uendeshaji ndani ya nusu ya pili ya mwaka wa fedha wa 2022.

Akizungumzia utendaji wa mwaka uliopita, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema mapato ya uendeshaji ya kampuni yaliongezeka kwa asilimia 14.3% Sh. bilioni 924.0 kutoka Sh. bilioni 808.7 mwaka 2020.

Alisema ukuaji huo ulitokana na ongezeko la asilimia 11.3 ya mapato ya jumla ya riba yaliyotokana na ukuaji wa mikopo kwa wateja wadogo na wakati, pamoja na ukuaji wa mikopo ya benki hiyo ikifunga mwaka na uwiano wa mikopo chechefu ya asilimia 3.3 kulinganisha na kiwango cha udhibiti cha soko kwa asilimia tano.

Nsekela alisema benki hiyo pia ilirekodi ukuaji mkubwa wa mizania wa mwaka hadi mwaka wa asilimia 23 kutoka Sh. trilioni 7.2 mwaka 2020 hadi Sh. trilioni 8.8, uliosababishwa na ukuaji wa asilimia 19.4 wa amana za wateja hadi Sh. trilioni 6.5 kutoka Sh. trilioni 5.4 zilizoripotiwa mwaka 2020, na ukuaji wa 20.6% wa fedha za wanahisa.

Nsekela alisema kipaumbele cha benki hiyo ni kuimarisha vichocheo vya ukuaji, na kujenga misingi imara ya uendelevu. Na kuwa mwaka wa fedha wa 2022 ndio wa mwisho wa mkakati wa muda wa kati ambao ulikuwa na jukumu muhimu katika kuimarisha utendaji, na umeipa msingi mzuri benki hiyo kukabiliana na siku zijazo.

Akizungumzia malipo ya gawio hilo, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa Benki hiyo na Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, alieleza kufurahishwa kwake na kuendelea kuongezeka kwa gawio huku akibainisha kuwa ukuaji huo ni mkubwa kupata kutokea. Dk. Kimei alisema kuwa hisa za benki hiyo zimebakia kuwa chachu ya wawekezaji kwasababu benki hiyo haijawahi kushindwa kutoa gawio kwa wanahisa wake.

# Mbeya waonyeshwa fursa za kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA na wajasiriamali mkoani Mbeya wameonyeshwa fursa mbalimbali za kibiashara.

Wapelekewa fursa hizo baada ya kukutana na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kama wateja wake wadogo na wakubwa wa jijini Mbeya ili kujadili fursa za biashara, kutambulisha huduma mpya za benki hiyo sambamba na kuwaelimisha wateja hao kuhusu faida na manufaa ya huduma hizo. Benki hiyo pia ilitumia fursa hiyo kujadili na wateja hao namna inavyoweza kuboresha huduma zake kulingana na mahitaji yao.

Akizungumza wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na benki hiyo mwishoni mwa wiki kupitia huduma yake ya NBC Biashara Club, Mkuu wa Kitengo cha Wajasiriamali wa Benki hiyo, Mussa Mwinyidaho, alisema Benki ya NBC imedhamiria kuboresha huduma zaidi ili wateja wake waendelee kufurahia huduma zilizorahisishwa zaidi ili kuendana na matakwa ya shughuli zao ili waweze kukuza biashara zao.

"Kupitia NBC Biashara Club tumekuwa na mkakati mpana wa kuwainua wajasiriamali kwa kuwajengea uwezo wa kibiashara kupitia semina za mafunzo, kuwasogezea huduma za kibenki, kuwajengea mitandao ya kibiashara pamoja na kuwapa mbinu za kurasimisha biashara zao ili waweze kukopesheka. Mpango huu umekuwa na tija si tu kwa wateja wetu bali pia hata sisi kama benki tumeweza kupata mrejesho uliotuwezesha kuboresha huduma zetu kwa ajili yao," alisema.

Alisema kupitia klabu hiyo, benki hiyo imeweza kutangaza huduma mpya kwa ajili ya wajasiriamali ikiwamo huduma ya 'Commercial Property Financing' inayowawezesha wajasiriamali wenye majengo ya biashara kupata mikopo yenye marejesho nafuu sambamba na huduma ya 'Commercial Asset Financing' inayowawezesha wajasiriamali hao kukopa mitambo kwa ajili ya biashara na shughuli za ukandarasi. "Pia kupitia tukio hili la leo wateja wetu mkoani Mbeya watapata fursa ya kufahamu huduma zetu za mikopo bila dhamana ikiwapo huduma ya 'Distributor financing' inayowawezesha wajasiriamali kupata mikopo ya kusambaza bidhaa zao bila dhamana pamoja na huduma ya 'Purchasing Order Financing' inayowawezesha wajasiriamali kupata mikopo kwa kutumia Hati ya manunuzi yaani LPO ," alisema.

Mwinyidahao alibainisha kuwa kupitia huduma ya NBC Biashara Club benki hiyo imeweza kuwakutanisha wanachama wa klabu hiyo na watoa huduma mbalimbali katika sekta ya biashara zikiwamo taasisi za serikali kama TRA, BRELA, TBS na nyingine nyingi ili kujadili na kutatua changamoto na kupata mafunzo zaidi kwenye masuala muhimu ikiwamo elimu kuhusu kodi.

Akizungumza kwa niaba ya wateja hao, Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Masoko (TCCIA) Mkoa wa Mbeya, Erick Sichinga, mbali na kuonyesha kuunga mkono mapinduzi ya huduma za kibenki kupitia Benki ya NBC alisema wafanyabiashara mkoani humo wameridhishwa kwa kiasi kikubwa na mchango wa huduma ya NBC Biashara Club kwa kuwa kupitia klabu hiyo wameweza kupata mafunzo ya kibiashara sambamba na kuelimishwa kuhusu fursa mpya za masoko na biashara.

"Suala la benki kubuni huduma mpya ni jambo moja ila kuhakikisha huduma hiyo inaeleweka na inatumiwa vema na walengwa ambao ni sisi wateja nalo jambo zuri zaidi. Tunashukuru sana NBC kwa kuwa si tu wanabuni huduma zinazotugusa bali pia wamekuwa wakihakikisha tunapata uelewa wa kutosha kuhusu huduma hizo kupitia huduma hii ya NBC Biashara Club," alisema.

Alisema hatua hiyo imekuwa msaada mkubwa kwa wafanyabiashara hao kwa kuwa imekuwa ikiwawezesha kufanya uamuzi sahihi kuhusu huduma mahsusi zinazoendana na aina ya biashara zao," alisema.




Mkuu wa Kitengo cha Wajasiriamali wa Benki ya NBC, Mussa Mwinyidaho (wapili kulia), akibadilishana mawazo na wageni waalikwa akiwamo Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Masoko (TCCIA) Mkoa wa Mbeya, Erick Sichinga (wapili kushoto), katika hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na benki hiyo mwishoni mwa wiki kwa ajili ya wateja wadogo na wakubwa wa jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yavutia wawekezaji wa Uswisi

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imewakaribisha wawekezaji kutoka Uswisi kuja kuwekeza nchini kwenye sekta mbalimbali.

Aliyetoa mwaliko huo ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambaye anasimamia uwekezaji, Ally Gugu akizitaja baadhi ya sekta za kuwekeza ni za uchumi.

"Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji hapa nchini (TIC) imefungua milango kwa wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania. Zipo fursa lukuki katika sekta mbalimbali za uchumi kwa mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ni mazuri," alisema Gugu.

Akizungumza baada ya kufanya mazungumzo na ugeni wa wafanyabiashara kutoka Uswisi ulioambatana na Balozi Uswisi hapa, Didier Chassot , Gugu mbali ya kupongeza ujio wao hapa nchini, aliwahakikishia kuwa Tanzania chini ya uongozi wa Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imejipanga kupokea wawekezaji kutoka nchini Uswisi.

"Tanzania ni nchi iliyojaliwa rasilimali nyingi na fursa nyingi kwenye uwekezaji na bisahara. Naomba nichukue fursa hii kuwakaribisha kuja kuwekeza hapa nchini Tanzania," alisema Naibu Katibu Mkuu.

Gugu alibainisha kuwa serikali itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutengeneza sera maalumu inayosimamia wafanyabiashara na wawekezaji wadogo ili sekta hizo ziweze kuleta tija zaidi na mchango stahiki katika maendeleo.

"Tunatambua kuwa wenzetu mmepiga hatua kubwa kwenye viwanda na sisi kama taifa tumedhamiria kujenga uchumi unaotegemea viwanda hivyo ni fursa kwa wawekezaji kutoka Uswisi kuja kujenga viwanda kwani tuna malighafi za kutosha nchini," alisema.

Balozi Chassot aliweka wazi dhamira ya ujumbe huo kuja nchini ni kujionea fursa zilizopo ili waweze kuzitumia na kuweka wazi jicho kuwa lao lipo kwenye sekta za biashara, viwanda, kilimo na utalii.

"Ni furaha kubwa kwetu kuwa hapa, na niseme wazi kuwa tumevutiwa na mazingira mazuri yaliyowekwa na serikali na kwetu hii inatupa picha nzuri kuja kuwekeza hapa," alisema Balozi Chassot.

Kwa mujibu wa Balozi Chassot, ujumbe wake utakuwa mabalozi wazuri wa kwenda kuzitangaza fursa zilizoko Tanzania na kuwahamasisha wenzao kuja kwa wingi kuwekeza Tanzania.

Naye Kaimu Mkurugenzi TIC, Mafutah Bunini, alisema ujio wa wageni hao ni sehemu ya kazi nzuri inayofanywa na serikali ya kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji na biashara zilizopo nchini.

# Washtakiwa wa mauaji wakutwa na kesi ya kujibu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imewaona washtakiwa wote watatu ambao wabashtakiwa kwa kosa la mauaji ya January Kasuhuke kwa kukusudia kuwa wana kesi ya kujibu baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wake.

Washtakiwa hao ni Juma Gulaka, Juma Kasanana na Bahati John. Uamuzi huo ulitolewa na Jaji wa Mahakama hiyo, Liliani Itemba.

Wanashtakiwa kwa kumuua January kwa kukusudia kwa kumcharanga mapanga shingoni, kichwani na mguu wake wa kushoto na kufariki dunia papo hapo na wapo mahabusu katika gereza la Geita kwa sababu kosa linalowakabili la mauaji halina dhamana.

Jji alisema upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa serikali James Pallangyo ulipeleka mashahidi 9 na vielelezo 7 ambavyo vimeonyesha kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo.

Jaji Itemba alisema ushahidi wote uliyotolewa na mashahidi wa upande wa Jamhuri unaonyesha washtakiwa wote kwa pamoja walishiliki kumuua January kwa kumcharanga mapanga kichwani, shingoni na mguu wake wa kushoto na kufariki dunia papo hapo, hivyo wanatakiwa wajitetee.

Mbali na Pallangyo na Jamhuri pia iliwakilishwa na Wakili Monika Matwe wakati upande wa utetezi wa washtakiwa ulikuwa ukiongozwa na mawakili watatu wa kujitegemea ambao ni Laurent Bugoti, Erick Rutehanga na Nestory Kuyula kila mmoja anamtetea.

Awali akisoma hati ya mashtaka Msaidizi wa kumbukumbu wa Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Ignas Kalihamwe, alidai Februari 3, 2010 katika msitu wa Samina Mkoa wa Geita washtakiwa wote kwa pamoja walimuua kwa kukusudia January kwa kumcharanga mapanga shingoni, kichwani na mguu wake wa kushoto na kufariki dunia papo hapo.

# TBS yatakiwa kwenda kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetakiwa kuwekeza katika vifaa na mifumo ya kidijitali ili kuendana na mapinduzi ya nne ya viwanda katika kuhakikisha ubora wa vipimo unaendelea kuthibitishwa.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Kanali Denis Mwila, wakati akisoma hotuba kwa niaba Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, kwenye Maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani ambayo yalifanyika Mei 20, mwaka huu mkoani hapa.

Alisema wale wanaotumia, kuendesha mashine ama vifaa katika sehemu za kazi wana wajibu mkubwa wa kujifunza na kuelewa vema teknolojia hiyo ya kidijitali ili waweze kuendesha na kutumia vyema mashine/vifaa hivyo katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Nawashauri wazalishaji, mamlaka za usimamizi wa ubora, hospitali, wafanyabiashara na wananchi wote kutumia vipimo sahihi ili tuweze kukuza uchumi wetu na ni matumaini yangu baada ya maadhimisho haya tutaenda kuchukua hatua stahiki katika matumizi bora ya vipimo," alihimiza Mwila.

Alitolea mfano wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kwamba hivi karibuni limetangaza kuanza kwa matumizi ya mita janja (Smart Meters) kwa wateja wao.

"Mita hizi zitafanya kazi kama simu janja au ving'amuzi vya luninga, ukishanunua Luku umeme utawaka moja kwa moja na hautahitajika kuingiza tena namba ili umeme uwake, mapinduzi haya ya teknolojia ya kidigitali yanapaswa kuhakikiwa ubora wake kwa kupimwa pia," alisema.

Alisisitiza kuwa sayansi ya vipimo ina umuhimu mkubwa katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, nishati, viwanda, taaluma, utafiti, afya na mazingira.

Alisema hiyo ni kwa sababu sayansi ya vipimo husaidia na huwezesha kuwa na ulinganifu wa vipimo duniani, ugunduzi na uvumbuzi wa kisayansi, uzalishaji viwandani, biashara ya haki na sahihi kati ya nchi na nchi na kupunguza vifo vya ajali na majeruhi kwa kutumia vifaa vya kupimia mwendo (traffic radar).

Aidha, alisema husaidia kutathmini ubora wa bidhaa, ulinzi wa biashara, afya na mazingira, na kuongeza imani kwa walaji na watumiaji.



Meneja wa Kampuni ya Madini ya Barrick nchini, Georgia Mutagahywa, akizungumza kwenye jukwaa la kwanza la utekelezaji wa ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini lililofanyika jijini Mwanza, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwongozo watolewa matumizi ya nyuki kwenye kilimo, ufugaji

**Na Neema Hussein, KATAVI**

SERIKALI imezindua mwongozo wa namna ya kutumia makundi ya nyuki kwenye huduma za uchavushaji wa mimea na mazao shambani utakaowasaidia wakulima na wafugaji nyuki nchini kupata manufaa zaidi kuliko kupata asali tu.

Akizungumza baada ya kuzindua mwongozo huo, Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, anasema mwongozo huo utasaidia wafugaji na wakulima kubadirika na kumuona mdudu nyuki kuwa ana thamani kubwa na kufanya kila linalowezekana kuweza kumtumia vizuri ili kujiongezea kipato.

Kwa kuonyesha ukweli kwamba uchavushaji ni kipato, Pinda anatoa mfano wa faida inayopatikana kwa mkulima na mfugaji nyuki anayekodisha makundi yake ya nyuki kwa mkulima mwingine.

Amasema mfugaji nyuki anaweza kuwakodisha wakulima wengine mizinga ya nyuki kwa kipindi cha msimu mmoja wa zao ambapo uzalishaji wa zao husika utaongezeka na mfugaji nyuki akilipwa ada ya uchavushaji huku pia uzalishaji wake wa mazao ya nyuki ukiongezeka maradufu. "Ziko nchi nyingine kwa kutambua kuwa nyuki ni wachavushaji wakuu wanaotoa uhakika wa chakula wameiweka sekta hii chini ya Wizara ya Kilimo, tubadilike tukifanya vizuri kwenye ufugaji nyuki tutakuwa na uhakikia wa chakula lakini nchi nyingi tutazishinda kwa uzalishaji asali,

"Sisi hapa tunauwezo wa kuzalisha hadi tani 140,000 na kuendelea kwa utajiri tulionao tatizo tu ni kwamba hatujafunguka licha ya serikali kuonyesha dhamira ya wazi ya kutaka kukuza sekta ya ufugaji nyuki," anasema Pinda.

Dk. Ezekiel Mwakalukwa, Mkurugenzi wa misitu na nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii nchini anasema mwongozo huo ni mkakati wa kuwasaidia wafugaji nyuki kuanzia kwenye uandaaji wa makundi ya nyuki, utunzaji wake wakiwa shambani hadi namna ya kuingia makubaliano. Miongoni mwa vipengele ambavyo mwongozo huo unaelezea ni namna ya kuandaa makundi ya nyuki kwa ajili ya uchavushaji, usimamizi wa makundi hayo ya nyuki yakiwa shambani, utaratibu wa kuyarudisha makundi ya nyuki baada ya uchavushaji mahali unapoyatunza, usalama na huduma ya kwanza katika shamba linalopata huduma ya uchavushaji na masula ya kuzingatia wakati wa kupanga bei ya ukodishaji makundi ya nyuki.

"Wadau wanapaswa kuuelewa mwongozo huu, na ni lazima kuufuata lakini huu ni mwongozo wa kwanza kutolewa hivyo tunaimani unaweza ukawa na mapungufu, hivyo basi tunakaribisha maoni ya wadau kwa jinsi watakavyokuwa wakiutumia," alisema. Mkurugenzi Mwakalukwa amesema mwongozo huo umezinduliwa baada ya tafiti kuonyesha kulikuwapo na uendeshwaji wa bishara ya kukodisha makundi ya nyuki pasipo kuwa na utaratibu.

Baadhi ya wafugaji nyuki wamesema, mwongozo huo umekuja wakati muafaka na unaonyesha wazi dhamira ya serikali katika kuwakomboa kiuchumi wafugaji nyuki nchini. Tulizo Kilaga anaripoti.

# Wadau utalii Arusha wapewa mbinu ya mikopo

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Francis Michael, amewataka wadau wa utalii mkoani Arusha kutumia fursa ya mikopo nafuu ya Benki ya NMB katika kuwekeza kwenye sekta ya utalii ili kuvutia wageni nchini.

Akizungumza katika kongamano la utalii (Tourism Networking) lililofanyika jijini Arusha mwishoni mwa wiki, Dk. Michael alisema Benki ya NMB imekuwa chachu katika kuhakikisha inawapa mikopo wadau wa sekta ya utalii katika kuimarisha mazingira ya vivutio nchini.

"Tunaomba mfanye jitihada za kuijenga sekta ya utalii kwani serikali imeshaweka mazingira ya kuitangaza kupitia filamu ya Royal Tour ambapo hadi sasa kuna baadhi ya hoteli zimeshajaa wageni, hivyo ni kitu cha kujivunia kwetu na nyie kama wadau ni vyema mkatumia fursa hiyo katika kuweka mazingira sawa," alisema Dk. Michael.

Dk. Michael aliwaeleza wadau wa utalii kutumia vema fursa waliyopewa na benki hiyo kwa sababu ni taasisi muhimu ya kifedha inayoshiriki kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kiuchumi na ubunifu nchini.

Alisema, fedha watakazotengewa kwa ajili ya mikopo wazitumie vema ili wazirudishe na wengine wapate fursa ya kuzipata kwa ajili ya kukuza uchumi na kuongeza idadi ya watalii nchini kwa maendeleo ya sekta zote.

"Hiki kinachofanywa na NMB ni kitu kikubwa sana, kifikirieni na mkitumie vizuri kwa sababu fursa kama hizi haziji mara mbili. Wafurahisheni watalii ili wakienda kwao wakawalete watu wengine na wao warejee tena na tena," alisema Dk. Michael.

Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa NMB, Filbert Mponzi, alisema benki hiyo wanaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kuboresha sekta ya utalii nchini.

"Tunafanya kila namna kuhakikisha tunaunga mkono maono ya Rais Samia. Utalii ni sekta muhimu katika uchumi wa nchi yetu, hapa katikati kulitokea mtikisiko mkubwa wa UVIKO-19 ambao ulikimbiza watalii, lakini sasa hakuna sababu ya kushindwa kutumia fursa ya vivutio tulivyo navyo kuwarudisha waje nchini, hasa baada ya Rais Samia kutufungulia njia kupitia filamu ya Royal Tour," alisema Mponzi.

Aidha, Mponzi alisisitiza kuwa kwa miaka ya hivi karibuni NMB imeanza kutoa huduma ya mikopo katika sekta ya utalii lengo ni kuimarisha katika kutoa huduma kwa wageni wanaofika nchini kutalii na kuona vivutio vilivyopo nchi nzima.

"Bado tunaendelea kutoa katika sekta ya utalii kwa lengo la kufanya vizuri zaidi na sasa tumejipanga kuwahudumia wageni wote wanaofika nchini, ili wakirudi kwao wapate sababu ya kurejea tena nchini," alisema Mponzi.

Nipashe
Spotika



SABABU 5, MADRID INA NAFASI KUBEBA UEFA KULIKO LIVERPOOL UK. 12-13



DEPAY

# WA5 WANAOTAKA KUONDOKA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wanatarajiwa kufanyia marekebisho makubwa ya kikosi katika majira ya joto. Kocha Xavi Hernandez anataka kukirekebisha kikosi chake na kushughulikia mapungufu yake ili kuleta changamoto mpya msimu ujao.

Tunatarajia kuona uhamaji wa aina yake pale Barcelona msimu huu wa majira ya joto. Wachezaji kadhaa wamehusishwa na kuondoka Camp Nou. Baadhi ya wachezaji hao wanaonekana kutokuwa na nafasi halisi ya kupata muda wa kucheza mara kwa mara au kufanikiwa wakiwa Barcelona.

Pia kuna wachezaji wachache ambao ni bora kucheza kwenye timu inayofaa zaidi kwa mtindo wao.

Hebu tuangalie wachezaji watano wanaohitaji kuondoka Barcelona msimu huu wa joto...

**#5. Samweli Umtiti**

Kimsingi, Samuel Umtiti alipaswa kuondoka Barcelona muda mrefu uliopita. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, ameshindwa kutambua uwezo wake kwenye Uwanja wa Camp Nou na jeraha lake la goti limekuwa sababu kubwa iliyochangia.

Barcelona wamekuwa wakitaka kumtoa kwa muda mrefu sasa. Kwa mujibu wa ripoti ya Mundo Deportivo (kupitia Marca), Umtiti alibubujikwa na machozi alipokuwa akimsihi rais wa klabu, Joan Laporta kutomuuza msimu uliopita wa majira ya joto.

Umtiti amecheza mechi moja pekee kwenye mashindano yote akiwa na Barcelona msimu huu. Iwapo Mfaransa huyo anapanga kucheza soka, anatakiwa kuhamia klabu ya kiwango cha chini kwani ndoto zake na Barcelona haziwezi kutimia.

**#4. Clement Lenglet**

Diario Sport ilidai mapema mwezi huu kwamba Clement Lenglet huenda akaondoka Barcelona mwishoni mwa msimu. Beki huyo wa kati alijiunga na miamba hao wa Katalunya msimu wa majira ya joto wa 2018 kutoka Sevilla kwa euro milioni 36. Baada ya kung'ara katika misimu yake michache ya kwanza, kiwango chake kimeshuka sana.

Lenglet sasa hana nafasi mbele ya Gerard Pique, Ronald Araujo na Eric Garcia. Huku Barcelona ikiripotiwa kuwa tayari wamefikia makubaliano ya kumsajili Andreas Christensen kwa uhamisho huru, Lenglet haonekani kuwa sehemu ya mipango ya Xavi Hernandez kwa msimu ujao.

Ana mkataba na Barcelona hadi 2026, ambayo ina maana kwamba wataweza kupata kiasi kizuri cha fedha kupitia mauzo yake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ameanza katika mechi tisa pekee za LaLiga na Ligi ya Mabingwa msimu huu.

**#3. Riqui Puig**

Baada ya kuibuka kwa vipaji vya vijana vya hali ya juu kama Pedri, Gavi na Nico Gonzalez, Riqui Puig amekuwa mtu asiye na nafasi pale Barcelona. Mhitimu huyo wa akademi ya La Masia alishindwa kumvutia Ronald Koeman na sasa ameshindwa kujitetea mwenyewe chini ya Xavi Hernandez pia.

Kwa mujibu wa Mundo Deportivo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amegundua kuwa kuondoka Barcelona litakuwa jambo bora zaidi kwa maisha yake ya soka hivi sasa. Anatarajiwa kufikisha umri wa miaka 23 Agosti na anapaswa kucheza mara kwa mara ili kuongeza uwezo wake.

Mkataba wa sasa wa Puig na Barca unaisha mwaka 2023. Kwa hivyo, wana uwezekano wa kuwa tayari kumuuza msimu huu wa majira ya joto. Katika mechi 15 kwenye michuano yote akiwa na Barcelona msimu huu, Puig amefunga bao moja pekee.

**#2. Martin Braithwaite**

Kuwasili kwa Pierre-Emerick Aubameyang, kumemfanya Martin Braithwaite kuwekwa pembeni. Kwa mujibu wa ripoti ya Diario Sport, Braithwaite haonekani katika mipango ya Xavi Hernandez kwa sasa au siku zijazo.

Mshambuliaji huyo wa Denmark amekuwa akitumika kwa kiasi kidogo msimu huu na amecheza mara mbili pekee kwa Barcelona mwaka 2022. Alikuwa nje ya uwanja kati ya Agosti 30 na Januari 20 kutokana na jeraha la goti. Braithwaite amefunga mabao mawili katika mechi tano kwenye mashindano yote akiwa na Barcelona hadi sasa msimu huu.

Brighton ni mojawapo ya timu ambazo bado zinavutiwa na Braithwaite, lakini kuna shida, mshambuliaji huyo ana mkataba hadi 2024 na mshahara wa karibu euro milioni nne kwa mwaka, unamfanya kuwa kwenye wakati mgumu kununuliwa na timu nyingine.

**#1. Memphis Depay**

Memphis Depay alijiunga na Barcelona msimu wa majira ya joto wa 2021 kwa uhamisho wa bure. Mshambuliaji huyo wa Uholanzi alianza vema maisha katika klabu hiyo, lakini mchango wake umepungua katika kipindi cha pili cha msimu.

Jeraha la msuli wa paja na tatizo la kifundo cha mguu lilimfanya akose kucheza kwa takriban miezi miwili. Wakati aliporejea Februari, Barcelona walikuwa wameimarisha idara yao ya ushambuliaji kwa kiasi kikubwa.


Kuwasili kwa Ferran Torres, Pierre-Emerick Aubameyang na Adama Traore kulimaanisha kwamba nafasi ya Depay kwenye kikosi cha kwanza ilikuwa hatarini. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, hajaonekana kwenye mechi nyingi tangu wakati huo.

Kwa mujibu wa AS, Xavi amemwambia rais Joan Laporta kwamba, ana nia ya kuwabakisha Depay na Frenki De Jong katika klabu hiyo msimu ujao. Hata hivyo, Barcelona wako tayari kukubali ofa ya euro milioni 30 kwa Mholanzi huyo.

Depay anapaswa kufikiria kuondoka Barcelona kwani anaweza kuwa chaguo la kwanza kwa timu kubwa Ulaya. Hilo lingekuwa chaguo bora zaidi kwa mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United.

## ISIKUPITE

HADI inatwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu, Klabu ya RS Berkane ya Morocco, haikushinda hata mechi moja ya ugenini; Hatua ya Makundi ugenini, Simba 1-0 Berkane, Gendermarie 2-2 Berkane, Asec Mimosas 3-1 Berkane. Robo Fainali; Al Masry 2-1 Berkane, Berkane 1-0 Al Masry. Nusu Fainali; TP Mazembe 1-0 Berkane, Berkane 4-1 TP Mazembe. Fainali (Neutral Ground- Nigeria) ; Orlando 1-1 Berkane (Penalti 4-5).



Extra Time



BENZEMA

# SABABU TANO, MADRID INA NAFASI KUBEBA UEFA KULIKO LIVERPOOL

**PARIS,** Ufaransa

LIVERPOOL wanaweza kuongeza taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye kabati lao ambalo tayari lina mataji mengi msimu huu, lakini wapinzani wao Real Madrid si wa kuwachukulia poa.

**Liverpool walishinda taji la FA Mei 14, mwaka huu, kwa kuifunga Chelsea baada ya dakika 120, pia wakiwa wamewafunga hao hao kwenye fainali ya Kombe la Carabao.**

Vijana wa Jurgen Klopp walishinda kwa mikwaju ya penalti na kulibeba Kombe la FA kwa mara ya kwanza baada ya miaka 16.

Liverpool imekuwa moja ya timu zinazotawala zaidi barani Ulaya msimu huu. Wamefanya vema katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini safari ya Real Madrid hadi fainali imekuwa ya majaribio zaidi.

Real Madrid imezitoa Paris Saint-Germain, Chelsea na Manchester City katika hatua ya mtoano. Katika kila moja ya mechi hizo, kuna wakati Real Madrid walionekana kabisa kushindwa. Lakini wameonyesha uwezo wa ajabu wa kuibuka kidedea mbele ya matatizo.

Hapa tunaangalia sababu tano kwa nini Real Madrid wana nafasi kubwa zaidi ya Liverpool katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itakayopigwa Mei 28, mwaka huu, twende sasa...

## #5. Msimu mrefu na mgumu zaidi kwa Liverpool

Liverpool wamebeba Kombe la Carabao na FA. Wameshinda mashindano yote mawili ya ligi ya nyumbani na sasa wanakimbizana na Manchester City kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England.

Liverpool walikuwa wamepitwa pointi moja na Man City kabla ya mechi moja moja za mwisho jana za Ligi Kuu msimu huu. Umekuwa msimu wa kufurahisha na wenye mafanikio tayari, lakini umekuwa wa kuchosha kwao.

Hadi Liverpool watakapocheza na Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa, watakuwa wamecheza takriban idadi ya juu zaidi ya michezo msimu huu. Hilo litawaumiza sana wachezaji na kunaweza kuwa na akili zilizochoka na miguu iliyochoka kule Stade de France Jumamosi wiki hii.

## #4. Wasiwasi wa ufiti wa wachezaji muhimu Liverpool

Mohamed Salah alitolewa katika kipindi cha kwanza cha fainali ya Kombe la FA dhidi ya Chelsea. Ili kufanya mambo kuwa mabaya zaidi, mlinzi mkuu wa Liverpool, Virgil van Dijk, pia alilazimika kutolewa nje baada ya mchezaji huyo.

Klopp amepuuza ukubwa wa majeraha, lakini hadi uchunguzi rasmi utakapofika, mashabiki wa Liverpool wanaweza kutarajia mabaya zaidi. Liverpool pia hawakuwa na kiungo mkabaji, Fabinho kwenye fainali ya Kombe la FA.

Alipata jeraha la misuli katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Aston Villa kwenye Ligi Kuu Mei 11. Liverpool inawafikiria wachezaji wake hao watatu muhimu kuelekea mchezo wao mkubwa zaidi msimu huu.

## #3. Matarajio makubwa, presha kubwa Liverpool

Kikosi cha Liverpool ni moja ya vikosi bora zaidi kwa zama hizi nchini England. Jurgen Klopp amewabadilisha kabisa. Kama si kwa timu yenye vipaji vya ajabu na iliyojikusanya kama Manchester City, Liverpool ingekuwa tayari imeshatwaa ubingwa wa England.

Kuna shinikizo kubwa kwa Liverpool kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Tunafahamu vema utaratibu wa vyombo vya habari vya Uingereza kwa kushabikia timu zao. Kupoteza fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Real Madrid kwa mara ya pili ndani ya miaka minne kutawapa shinikizo kubwa lisilopendeza na lisilostahili.

Lakini je, Liverpool wataweza kuimarisha hadhi yao kama moja ya timu bora kwa soka la kisasa?

## #2. Real Madrid wapo juu ya Liverpool, Klopp mwaka 2018 na 2021

Katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2017-18, Real Madrid iliichapa Liverpool mabao 3-1. Mpira wa tik-taka wa Gareth Bale na jeraha la Mohamed Salah na makosa ya golikipa wa Liverpool, Loris Karius yalipeleka huzuni kule Anfield.

Liverpool walikuwa na mambo machache ambayo yamewaendea mrama usiku huo na walikuwa wamedhamiria kulipiza kisasi wakati pande hizo mbili zilipopambana tena msimu uliopita. 'Wekundu' hao walikutana na 'Blancos' hao katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita.

Real Madrid ilishinda kwa jumla ya mabao 3-1 na kuwaondoa wachezaji wa Klopp katika michuano hiyo mikubwa barani Ulaya. Wakiwa wameshinda mechi mbili muhimu dhidi ya Liverpool siku za hivi karibuni, Real Madrid bila shaka watakuwa na nafasi kubwa kwenye fainali ya Mei 28, mwaka huu.

## #1. Real Madrid ndio wafalme wa Ligi ya Mabingwa Ulaya

Real Madrid wamelazimika kuvuka njia ngumu sana ya kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa. Kwa kweli, wamethibitisha katika awamu ya mtoano kwamba, kile wanachokiita "urithi wa Ligi ya Mabingwa" ni kweli kabisa.

Wametawazwa mabingwa wa Ulaya mara nne katika muongo mmoja uliopita. Real Madrid ilizishinda timu tatu bora zaidi katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa msimu huu. Walitoka nyuma na kuwashinda PSG, Chelsea na Manchester City.

Real Madrid walikuwa nyuma kwa mabao mawili dhidi ya Manchester City hadi dakika 90 za mchezo. Walifunga mabao matatu na kuondoa ndoto ya kikosi cha Pep Guardiola kunyakua ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Karim Benzema ameibuka kidedea kwa Real Madrid katika michezo yote hiyo. Alifunga hat-trick ya dakika 17 katika mchezo wa pili wa hatua ya 16-bora dhidi ya PSG. Mfaransa huyo alifuatia kwa kufunga hat-trick dhidi ya Chelsea katika mchezo wa kwanza wa robo fainali.

Alifunga bao la ushindi dhidi ya 'Blues' hao katika mchezo wa pili pia. Benzema kisha akafunga mabao mawili katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali dhidi ya Manchester City. Alitoa pasi ya bao la ushindi kwa vijana wa Carlo Ancelotti katika dakika ya tano ya muda wa nyongeza katika mechi ya pili.

Hizi ni aina za hadithi zinazofaa. Benzema na timu hii ya Real Madrid ni ngumu kuwasimamisha.

## Nukuu

"Nina furaha sana. Hapa naweza kuendelea kukua ndani ya klabu kama Paris ambayo inatoa kila kitu kufanya kwa kiwango cha juu zaidi. Pia nina furaha sana kuweza kuendelea kuwa Ufaransa, nchi nilikozaliwa, nilikulia na kustawi. Hapa ni nyumbani kwangu, mji wangu kama ninavyosema siku zote. Nitaendelea na Paris Saint-Germain kushinda mataji pamoja," **Kylian Mbappe baada ya kusaini mkataba mpya utakaomweka PSG hadi mwaka 2025.**




"Dhidi ya Liverpool hii huwezi kushinda ligi mwezi mmoja uliopita au mechi mbili au tatu zilizopita. Lazima upigane hadi mwisho. Liverpool ni moja kati ya timu bora zaidi ambazo nimewahi kuziona maishani mwangu," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.**



"Kushinda tuzo hii kwa mara ya pili ni mafanikio ambayo ninajivunia sana, nadhani uchezaji wangu msimu huu umekuwa mzuri na nina furaha kwamba nimeweza kuchangia mabao na pasi za mabao kwa msimu mzima," **Kiungo wa Manchester City, Kevin de Bruyne baada ya juzi kuchaguliwa kuwa mchezaji bora wa msimu wa 2021-22 wa Ligi Kuu ya England.**





Kiungo wa Simba, Jonas Mkude, akijaribu kumlamba chenga mchezaji wa RS Berkane Hamza Regragui, kwenye mechi ya makundi, Kombe la Shirikisho Afrika Machi 13, mwaka huu, ikishinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# WACHEZAJI WANAOTAKIWA KUTUA SIMBA ITISHE CAF

**Na Adam Fungamwango**

KUNDI D ambalo walikuwapo wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), Simba ndilo lililotoa bingwa wa michuano hiyo.

**RS Berkane ya Morocco ndiyo mabingwa wapya wa Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuifunga Orlando Pirates ya Afrika Kusini kwa mikwaju ya penalti 5-4 Ijumaa kwenye Uwanja wa Godswill Akpabio nchini Nigeria. Ni baada ya timu hizo kutoka sare ya bao 1-1 kwa dakika 120.**

Orlando Pirates iliiondosha Simba kwenye hatua ya robo fainali kwa mikwaju 4-3 ya penalti katika Uwanja wa Orlando, Soweto nchini Afrika Kusini. Na hii ni baada ya wenyeji kushinda bao 1-0 siku hiyo Aprili 24, wakati Aprili 17 ilifungwa bao 1-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam hivyo kuwa sare ya bao 1-1.

Mabingwa wapya wametoka kwenye Kundi D na kumaliza wakiwa vinara kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa dhidi ya Simba, zote zikiwa na pointi 10.

Timu zingine zilizokuwa kwenye kundi hilo ni ASEC Mimosas ya Ivory Coast na US Gendamarie ya Niger. RS Berkane iliifunga Simba mabao 2-0 Februari 27, kabla ya Wekundu wa Msimbazi kulipiza kisasi kwa kushinda bao 1-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Machi 13, mwaka huu.

Hata msimu uliopita, Simba ilikuwa Kundi A na timu iliyomaliza kuwa Mabingwa wa Afrika, Al Ahly, tena ikitoka kuongoza kundi ikiwa na pointi 13, Waarabu wakishika nafasi ya pili kwa pointi 11.

Msimu huu inaonekana baadhi ya wachezaji wake wengi wameshuka viwango, kuridhika na mafanikio na wengine kuwa na viwango visivyoendana na ukubwa na timu. Ni wachezaji wa aina gani ambao wanatakiwa kwenye kikosi hicho ili kirejee msimu ujao na kuwa imara?

**#1. Beki wa pembeni**

Simba inatakiwa kutafuta mabeki wa pembeni, kushoto na kulia ili kuwasaidia Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Shomari Kapombe ambao wanaonekana kucheza mechi nyingi mfululizo za ndani na kimataifa bila kupumzika, hivyo kuchoka. Wanatakiwa kutafutiwa wasaidizi wa nguvu na si wa kubabaisha, wenye uwezo wa kucheza mechi za kimataifa.

Mabeki hao wawe na uwezo kuwazidi waliopo, au kuwa sawa nao, iwe kutoka ndani au nje ya nchi. Kama si hivyo, basi kusajili beki mmoja mwenye uwezo wa kucheza sehemu zote mbili, kushoto na kulia.

**#2. Beki wa kati**

Kwa muda mrefu, Simba imekuwa ikifungwa mabao mengi ya kona, faulo na krosi. Baada ya ujio wa Joash Onyango, ilionekana kama tatizo limekwisha kwa sababu alikuja kuondoa kabisa na likapungua. Hata hivyo, kadri siku zinavyozidi kwenda linaonekana kurejea. Pamoja na msimu huu kufanya usajili bora wa beki Henock Inonga, bado inaonekana kuna upungufu wa angalau beki mmoja, hasa namba tano ambaye atakuja kuituliza timu. Inatakiwa ipate beki mmoja mwenye kasi, mtulivu, kwenye uwezo wa kuchezea mpira, mwepesi, anayeweza kucheza au kuokoa mipira ya vichwa, kufuta makosa ya wenzake, pia kuanzisha mipira mirefu haraka, anapopokonya mipira kutoka kwa adui.

**#3. Kiungo mkabaji**

Hili ndilo tatizo kuu kwenye kikosi hicho kwa misimu kadhaa. Inavyoonekana ni kama vile wanaosajili kwenye klabu hiyo wanapenda sana wachezaji kwenye uwezo wa kuchezea mpira, kuliko wachezaji wagumu, wenye nguvu na uwezo wa kunyang'anya mpira.

Tangu kifo cha Patrick Mafisango aliyefariki 2012, bado Simba haijapata mbadala wake. Huyu alikuwa na uwezo mkubwa wa kukaba, na muda huo huo kwenda mbele kusaidia mashambulizi na kuwa mmoja wa wafungaji wazuri wa mabao kwenye klabu hiyo.

Wamekuja viungo wakabaji wengi, angalau Mbrazil Gerson Fraga alionyesha kuimudu kwa asilimia nyingi. Simba inakosa viungo wakabaji wa uhakika, hivyo kusababisha mabeki wake muda wote kuhenya kuzuia mashambulizi.

Haina 'wakata umeme' ambao waunaweza kusema watawafanya mabeki wapumzike na kufanya kazi chache msimu huu.

Ukiangalia timu kama TP Mazembe, Al Ahly na nyingine zinazocheza michuano ya kimataifa, wana viungo wakabaji wenye miili iliyoshiba, wanaoijua kazi yao vema. Na mara nyingi hadi timu za Waarabu viungo wakabaji wao huwatoa Afrika Magharibi kwenye nchi kama Burkina Faso, Nigeria, Cameroon, Ghana na zingine za jirani.

**#4. Kiuungo mshambuliaji, winga**

Pia ina mapungufu kwa mawinga wake ambao wamekuwa dhaifu kwa kufunga mabao na kupiga krosi za uhakika. Angalau Peter Banda amekuwa na uwezo wa kupiga krosi zinazofika eneo husika, lakini wengine akiwamo hata Bernard Morrison, bado wana tatizo hilo.

Mawinga wake pia hawana sanaa ya kufunga kama ilivyokuwa huko nyuma kwa kina Emmanuel Okwi, au Luis Miquissone ambao walishindana na matraika kutupia.

Ukiondoa Clatous Chama, ambaye hucheza kiungo mshambuliaji, mwenye uwezo wa kutoa pasi za mwisho, haina mwingine tena zaidi ya huyo.

**#5. Mastaika watatu**

Kwa uchache Simba inatakiwa kusajili mastraika watatu. Wawili wawe wa kigeni na mmoja wa ndani mwenye uwezo wa kufunga mabao.

Hili ni eneo ambao kwa kiasi kikubwa limewakosesha ubingwa Simba na kuwaondoa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ikaenda Shirikisho ambako nako ikaishia robo fainali. Waliopo sasa hawafungi. Vyovyote itakavyokuwa iwe kwa viwango kushuka au umri, lakini Meddie Kagere, John Bocco na Chris Mugalu ni kama wamefikia ukingoni.

## JE, WAJUA?



WAKATI msimu wa Ligi Kuu England 2021/22, ukifikia ukiongoni jana, Arsenal na Everton ndizo klabu zinazoshikilia rekodi ya wachezaji wake kuonyeshwa kadi nyekundu nyingi zaidi tangu ligi hiyo iingie kwenye uendeshwaji wa mfumo mpya 'Premier League'. Tangu Mikel Arteta aanze kuinoa ina kadi nyekundu 16, lakini kwa ujumla inazo 102 sawa na Everton zikifuatiwa na Chelsea - 82, Tottenham - 69 na Manchester United - 68.



# Familia zenye watoto wenye ulemavu zatakiwa ushirikiano sensa ya makazi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MRATIBU wa Mradi wa Elimu Jumuishi, Mkoa wa Dodoma, Janne Mgidage, amezitaka familia zenye watoto wenye ulemavu kutoa ushirikiano kwenye zoezi la Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu, ili serikali ipate taarifa sahihi zitakazosaidia kwenye mipango mbalimbali.

Mratibu huyo alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo.

Alisema taarifa za watu wenye ulemavu ni muhimu kwa serikali katika kupanga maendeleo yake ili kutowaacha nyuma.

"Wazazi au familia zenye watu wenye ulemavu zitoe ushirikiano kwa kuwa idadi yao itachangia wao kupata haki ya msingi kwenye mipango ya bajeti," alisema.

Alisema sensa hiyo ina manufaa makubwa kwa Watanzania, na hakuna sababu ya kuwaficha watoto wao maporini na majumbani ili wasiandikishwe.

"Familia hizo zihakikishe zinatoa idadi halisi ya hesabu za watu wanaoishi nao badala ya kuidanganya serikali kwa kutoa majibu yasiyo na tija ya manufaa ya nchi," alisema.

Hata hivyo, mratibu huyo alisema elimu bado inahitaji kwenye familia zinazoishi na wenye ulemavu, ili kuondokana na imani potofu ya kuwaona watu hao hawana haki ya kutambuliwa kama ilivyo kwa wengine.

Alisema kuwa kutokana na kukosa elimu hiyo makundi hayo ya watu wenye ulemavu wanaendelea kukosa haki zao za kimsingi kama vile ya kupata matibabu, chakula, malazi na elimu.



Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khadija Said, akisalimia na mmoja wa watoto yatima wanaolelewa na kituo cha kulelea cha Tosamanga chini ya usimamizi wa Kanisa Katoliki katika Wilaya ya Iringa, mkoani Iringa. TIRA walitembelea kituo hicho na kutoa msaada wa vyakula mbalimbali yakiwamo maziwa, mchele, maharagwe na nguo hivi karibuni. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Sera ya Wazee mbioni kukamilishwa Oktoba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, amemwagiza Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Nandera Mhando, kuhakikisha Sera ya Wazee inayoboreshwa ina kamilika Oktoba, mwaka huu.

Aidha, amewaasa wazee nchini kutunza afya zao kwa kujiepusha na mtindo hatarishi ya maisha.

Mpanju alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifunga mkutano wa viongozi wa mabaraza ya wazee kutoka mikoa ya Tanzania Bara.

Alisema kukamilika kwa sera hiyo kutaanzisha mchakato wa utungwaji wa Sheria ya Wazee.

"Kuna mengine mengi mmeyasema ila mengi ya hayo yanahitaji mwongozo wa Sera ya Wazee hivyo sera hii ikikamilika hayo mengine yatafanyika na kutekelezeka kwa ufanisi," alisema Mpanju.

Pia, alisema serikali itahakikisha wazee wanalindwa kwa kuweka mifumo kuwalinda na vitendo vya ukatili pamoja na kuwapa huduma bora za afya.

Alisema kuwa wazee wanapaswa kuhakikisha wanajitunza kiafya ili kutumika na taifa kwa kutoa ushauri wa kujenga uchumi wa nchi.

"Niwaombe wazee wangu tujitunze hasa katika afya zenu, afya ni muhimu sana kwani bado tunahitaji nasaha na mawazo yenu katika sekta mbalimbali ili tuweze kufikia maendeleo tuliyojiwekea kama taifa," alisema Mpanju.

Naye Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Amina Faki, alisema ofisi hiyo itahakikisha wazee wanapata huduma kwa kuzingatia sheria na sera.

"Katika kutoa huduma bora za afya, serikali imetenga madirisha 5,888 katika vituo vya kutoa huduma za afya kote nchini zikiwamo zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mkoa na rufani," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Taifa, Lameck Sendo, alisema mkutano huo umetoka na maazimio ambayo yakitekelezwa kwa ufanisi na weledi, wazee nchini watapata ulinzi na huduma muhimu kwa ustawi wao.

Alitaja maazimio mengine ni kuimarisha Baraza la Wazee Taifa, wazee kulindwa na vitendo vya ukatili, kushirikishwa katika masuala mbalimbali katika jamii, kufutwa kwa kodi mbalimbali kwa wazee na upatikanaji wa huduma bora za afya. Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shirika la Help Age, Daniel Smart, alisema shirika lake linaendelea kushirikiana na serikali katika ngazi mbalimbali kuhakikisha mabaraza ya wazee yanaundwa na kujiendesha.

# DIT yafurahia uboreshwaji miundombinu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Prof. Preksedis Ndomba, amesema ushindi alioupata Sandra Sommi, katika mashindano ya ubunifu kitaifa, umetokana na kuboreshwa kwa miundombinu kulikofanywa na taasisi hiyo.

Sandra ameshika nafasi ya kwanza upande wa vyuo vya kati baada ya kubuni kifaa cha kusaidia watoto wenye shida ya upumuaji, hususani njiti, katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Akizungumza baada ya Sandra kutangazwa mshindi, Prof. Ndomba alisema ushindi huo unazidi kuchochea hamasa ya wanafunzi kuendelea kubuni vifaa mbalimbali vinavyohitajika kwa ajili ya kutatua kero mbalimbali nchini.

Alisema kama taasisi wamefurahia ushindi huo, akisisitiza umetokana na miundombinu ambayo taasisi hiyo imeweka kwa ajili ya kuwaimarisha wanafunzi kimazoezi baada ya masomo ya darasani.

"DIT tumefurahi sana kuona mwanafunzi wetu amepata ushindi, ninampongeza sana yeye na wengine ambao waliwahi kushinda katika mashindano haya, tayari ameingia katika timu ushindi ya taasisi," Prof. Ndomba alisifu.

Alibainisha kuwa wanafunzi hao waliamua kubuni kifaa hicho na vingine baada ya kutembelea katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Amana na kufanya utafiti, walirejea chuoni na kuamua kubuni vifaa au mashine ambazo hutumika hospitalini kwa ajili ya kupunguza tatizo la upumuaji.

Alisema kifaa hicho ambacho kimepata ushindi, tayari kimefanyiwa majaribio ya awali na kuongeza kuwa wamewasiliana na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO) ambayo iko kwa ajili ya kuendeleza mitambo mikubwa ikiwamo kuzalisha vifaa vya tiba nchini.

"Wiki ijayo, TEMDO wanatarajia kuja kuiangalia kwa mara ya pili ili iweze kubiasharishwa na kuanza kutumika katika hospitali mbalimbali hapa nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema mwakani wanatarajia kuanzisha kituo cha kuzalisha mitambo mikubwa, ambayo itakuwa inaziboresha mashine ndogo kuwa kubwa.

Naye mshindi wa bunifu hiyo, Sandra Sommi alisema wazo la kubuni mashine hiyo alipewa na madaktari wa Muhimbili kutokana na uwapo wa tatizo la gharama za upatikanaji wa mashine za aina hiyo.

Alisema baada ya kurejea, waliamua kubuni kifaa hicho ambacho bado hawajaanza kukiuza kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa watoto wenye tatizo la upumuaji.





# Waomba ruzuku kwenye mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo hasa mbolea ili kupunguza makali ya bei ya bidhaa hiyo wakidai kuwa bei ya sasa inawakatisha tamaa ya kuendelea kulima.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo maalumu ya kilimo bora cha mpunga na matumizi sahihi ya mbolea yaliyotolewa kwa ushirikiano kati ya maofisa wa Kampuni ya Mbolea ya YARA Tanzania na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole.

Mafunzo hayo yalitolewa katika moja ya mashamba darasa yaliyoandaliwa na taasisi hizo kwenye skimu ya umwagiliaji ya Matebete ambayo inahudumia wakulima zaidi ya 800 wa Wilaya ya Mbarali.

Mwenyekiti wa skimu hiyo, Daud Mwalugamba, alisema bei ya mbolea msimu huu wa kilimo bei yake imekuwa juu kuliko miaka yote ambayo wamekuwa wakilima na kwamba bei hizo zimesababisha wakulima wengi kushindwa kulima kilimo cha kisasa.

Alisema miaka ya nyuma walikuwa wananunua mbolea ya kupandia kwa bei isiyozidi Sh. 65,000 lakini mwaka huu imepanda kwa zaidi ya mara dufu na imekuwa ikiuzwa Sh. 130,000 kwa mfuko mmoja wa kilo 50 huku mbolea ya kukuzia ambayo walikuwa wananunua chini ya Sh. 50,000 ikiuzwa kwa Sh. 120,000.

Alisema hali hiyo imekuwa ikitajwa kuwa imesababishwa na matatizo mbalimbali ikiwamo mlipuko wa virusi vya corona vilivyotikisa dunia nzima pamoja na vita kwenye mataifa yanayozalisha bidhaa hiyo, lakini akashauri serikali kuweka ruzuku.

"Miaka ya nyuma serikali ilikuwa inaweka ruzuku kwenye mbolea ndio maana ilikuwa haipandi bei, lakini kwa sasa bei iko juu kwa sababu hakuna tena ruzuku, tunamwomba rais wetu atusaidie kuweka ruzuku kwenye mbolea hizi," alisema Mwalugamba.

Naye Bonface Chonya alisema pamoja na matatizo ya bei ya mbolea kuwa juu lakini bado wanakabiliwa na tatizo la unyonyaji unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara kwa kutumia vipimo visivyokuwa rasmi wakati wa ununuzi wa zao hilo.

Aliiomba serikali kuweka utaratibu wa wanunuzi hao kununua mazao ya wakulima kwa kutumia mizani badala ya vifungashio ambavyo vinatumika kwa sasa.

Alisema wanunuzi wa zao hilo bado wanatumia lumbesa kununua zao hilo jambo ambalo limekuwa likipigiwa kelele mara kwa mara lakini bado halijapata ufumbuzi.

Ofisa Kilimo Kiongozi wa Kampuni ya YARA anayesimamia Tanzania na Burundi, Donat Fungu, alisema kampuni hiyo imekuwa ikiwauzia wakulima mbolea kwa bei nafuu ikilinganishwa na kampuni nyingine.

Alisema mbolea zinazouzwa na kampuni hiyo zinazalishwa nchini Tanzania na zina ubora wa hali ya juu kutokana na kuzalishwa kwa kuzingatia tafiti za udongo wa Tanzania na kwamba maofisa kilimo wa kampuni hiyo wako kila mkoa.

"Tumetoa elimu kwa kuitumia hili shamba darasa, tumewafundisha upandaji bora na matumizi sahihi ya mbolea, sasa tunachukua namba zenu za simu na tutawatembelea kwa kushtukiza ili kujiridhisha kama kweli mnafuata taratibu," alisema Fungu.



Ofisa Kilimo Kiongozi wa Kampuni ya YARA anayesimamia Tanzania na Burundi, Donat Fungu (kulia), akitoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wa skimu ya Matebete wilayani Mbarali, kampuni hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole wameandaa shamba darasa la kufundishia wakulima zaidi ya 800. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mgogoro wa ardhi wa vijiji watatuliwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imeumaliza mgogoro wa mipaka kati ya Kijiji cha Chokaa kilichoko Kata ya Mbugani na Itewe kilichoko katika Kata ya Sangambi ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 14.

Mgogoro huo uliibuka mwaka 2006 baada ya kuandaliwa ramani mpya ya vijiji hivyo ambapo kila upande wa vijiji hivyo ulikuwa unadai kuwa eneo la Sinjilili liko upande wake na hivyo kusababisha mvutano uliokuwa unahatarisha amani.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka Simon Mayeka, aliumaliza mgogoro huo mwishoni mwa wiki kwa kuzikutanisha pande zote mbili na kusikiliza kila upande kabla ya kutoa uamuzi ambao ulimaliza mgogoro huo.

Alisema baada ya kusikiliza pande hizo mbili alibaini kuwa mgogoro huo ulisababishwa na upimaji wa vijiji 21,000 uliokuwa umeandaliwa na serikali mwaka 2006.

Alisema vijiji hivyo vyote vipo ndani ya Mji wa Chunya na hivyo haitakiwi kuendelea na mfumo wa vijiji na badala yake inaandaliwa mitaa ili kuondoa mgogoro huo.

"Sasa hivi kinachogombaniwa ni kila upande kudai kwamba eneo hili lipo upande wake, sasa tukiweka mitaa hakutakuwa tena na vijiji na huu mgogoro utakuwa umekwisha kabisa, sasa hivi nimewataka wananchi wawe watulivu kwanza," alisema Mayeka.

Aliwataka wananchi hao kusubiri utaratibu wa kugawa vijiji vyote vilivyoko mjini na kuwa mitaa ili kuondoa migogoro hiyo huku akiwataka viongozi kutowachochea wananchi.

# Biashara vyuma chakavu yaleta shida

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BIASHARA ya vyuma chakavu imegeuka kuwa tatizo mkoani Mbeya kutokana na kudaiwa kuchochea uharibifu wa miundombinu ya umeme, barabara na madaraja kwa baadhi ya watu kuiba vyuma vinavyotumika kwenye miundombinu hiyo.

Kutokana na tatizo hilo, Jeshi la Polisi mkoani humo, limepiga marufuku uuzwaji wa vyuma hasa vilivyotengenezwa kwa madini ya shaba (copper) ambavyo ndivyo vinatumika kwenye ujenzi wa miundombinu hiyo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Ulrich Matei, aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya uharibifu wa miundombinu katika mkoa huo.

Alisema hivi karibuni jeshi hilo liliwakamata watu 12 ambao walikuwa wanahujumu miundombinu ya umeme na barabara kwa kuiba vyuma na nyaya za umeme kisha kwenda kuuza jambo ambalo alisema linahatarisha miundombinu hiyo. Kamanda Matei alisema jeshi hilo likishirikiana na maofisa wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), walifanya operesheni maalumu ya kuwasaka wahujumu wa miundombinu ya umeme na kuwakamata watu wanane wakiwa na baadhi ya vifaa vya shirika hilo.

Alisema baadhi ya vitu walivyokutwa navyo ni nyaya za umeme za TANESCO na baadhi ya vyuma vinavyotumika kujenga miundombinu hiyo ambavyo viliibwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

"Lakini tuliwakamata watu wanne ambao walikuwa wanahusika na wizi wa vyuma kwenye barabara ya Idiga-Umalila, hali hii imetulazimu kupiga marufuku biashara ya vyuma hivi na yeyote atakayekamatwa tutamshughulikia," alisema Kamanda Matei.

Alisema jeshi hilo litaendelea kushirikiana na taasisi zingine kufanya operesheni ya kuwasaka wahujumu wa miundombinu hiyo na kwamba wakikamatwa watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria ili kuwa fundisho.

Alisema serikali inatumia fedha nyingi kujenga miundombinu hiyo na hivyo inahitajika nguvu ya ziada kuilinda ili idumu na kuwasaidia wananchi kupata huduma kwa muda mrefu.

Kamanda Matei aliwaomba wananchi kuendelea kushirikiana na shirika hilo pamoja na taasisi zingine kulinda miundombinu kwa kutoa taarifa za siri kuhusu wahujumu wa miundombinu hiyo ili wakamatwe na kushughulikiwa.

Alisema miundombinu hiyo ni kwa ajili ya wananchi wenyewe na hivyo wanao wajibu wa kuilinda isiharibiwe na wahuni akisisitiza kuwa wao ndio watakuwa wa kwanza kupata madhara kwa kukosa huduma.

Hivi karibuni watu wasiojulikana walihujumu miundombinu ya umeme katika Wilaya ya Kyela ambayo ilikuwa inadaiwa kuwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 800 ambapo vyuma mbalimbali viliibwa.





Wanachama wa CCM na jumuiya zake wakisubiri kupiga kura kwenye uchaguzi wa jumuiya hizo katika tawi la Shangani mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# SMZ yaunda kikosi kazi kupitia mfumo wa elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeunda kikosi kazi kwa ajili ya kupitia muundo wa mfumo wa elimu ya juu ikiwamo sheria na sera pamoja na mitaala kwa ajili ya kufanya marekebisho yatakayoleta ufanisi wa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa.

Hayo yalisemwa jana mjini hapo na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya sekta ya elimu pamoja na matumizi ya fedha za ahuweni ugonjwa wa UVIKO-19.

Alisema lengo la kuundwa kwa kikosi kazi ni baada ya kubainika kuwapo kwa kasoro mbalimbali katika muundo wa sekta ya elimu ikiwamo mitaala na imebainika kushindwa kuleta ufanisi ikiwamo ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya elimu ya juu ya sekondari.

Alisema wanafunzi wa Zanzibar wanafanya mitihani ya elimu ya juu ya sekondari kuanzia kidato cha nne hadi cha sita ambayo hufanywa pamoja na wenzao wa Tanzania Bara, lakini ufaulu kwa upande wa Zanzibar hauridhishi.

Alizitaja kasoro hizo kwa kiasi kikubwa zimeibuwa malalamiko kutoka kwa makundi mbalimbali ikiwamo wadau wa sekta ya elimu na wazazi na ndiyo zilizoisukuma wizara kuunda kikosi kazi kuibua changamotohizo.

"Hizo ndiyo sababu ambazo zimeifanya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuunda kikosi kazi kuibua na kuzifanyia kazi changamoto zitakazoibuliwa na wataalamu hao," alisema.

Alisema kikosi hicho kitaongozwa na Mwenyekiti wake aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Professa Idriss Ahmada Rai, ambaye aliongoza chuo hicho kwa muda wa miaka 10.

Alisema Professa Rai amebobea katika mifumo ya sayansi na teknolojia ya kompyuta ambaye atakuja na jibu njia zipi za kuboresha elimu ya sayansi kwa wahitimu wa kuanzia elimu ya sekondari hadi vyuo vikuu na kuingia katika soko la ajira na kujiajiri.

Katika kikosi kazi hicho kimejumuisha wasomi waliobobea katika sekta ya elimu akiwamo aliyekuwa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ubungo. Pia Katibu Mkuu Wizara ya Elimu ya Kenya, Dk. Sara Ruto, amejumuishwa katika kikosi kazi hicho na Kenya tayari imefanya mageuzi makubwa ya mapitio ya muundo wa elimu na mitaala kwa ajili ya kuleta ufanisi mkubwa na kuwawezesha wahitimu wake kuingia katika soko la ajira.

Waziri Lela alisema pia katika kikosi hicho yumo mtaalamu wa lugha ya Kiingereza ambaye amehitimu Shahada ya Juu za Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Monash cha Australia, Mariyam Ismail Jaffar, ambaye kwa sasa ni Mhadhiri Mwandamizi wa SUZA.

Alisema kikosi kazi hicho pia kimepewa kazi ya kuangalia mfumo wa elimu wa vyuo vya amali Zanzibar kuona kwa kiasi gani unaweza kusaidia wahitimu wake ufaulu na kuajiriwa katika sekta mbalimbali.

Kadhalika, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari inakusudia kujenga vyuo vya amali vitano kwa ajili ya kuhakikisha wahitimu wake wanaingia katika soko la ajira bila ya matatizo.

"Kipaumbele katika mageuzi makubwa ya elimu kuona wahitimu wake wanaingia katika soko la ajira ni kujenga vyuo vya amali vitano katika kila mkoa wa Unguja na Pemba ikiwamo nyingine vilivyopo sasa ambavyo vinapokea wanafunzi," alisema. Alisema wizara yake imejipanga kikamilifu kuona wanafunzi wanakuwa na ufaulu bora katika masomo yao ya sekondari na jumla ya maabara za sayansi 10 zitajengwa kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi kufanya vizuri masomo hayo ikiwamo Fizikia, Kemia, Bailojia na Hisabati.

Katika hatua ya kuleta ufanisi, alisema Wizara ya Elimu ipo katika hatua za mwisho za kuajiri walimu 4,227 ambao watakwenda kusomesha katika shule ambazo zipo katika mchakato wa ujenzi wake huku walimu wa masomo ya sayansi wakipewa kipaumbele cha kwanza.

# Mpango uchumi wa buluu kusaidia matumizi endelevu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud, amesema kuwapo kwa mpango wa matumizi ya bahari ndiyo suluhu ya kuwa na matumizi mazuri na endelevu baharini.

Aliyasema hayo alipokuwa akifungua mkutano wa mpango wa matumizi ya bahari (Marine Spatial Planning MSP), uliofanyika mjini hapo.

Alisema katika bahari kuna rasilimali nyingi ambazo wanazitegemea, kuwa na mpango huo utaelekeza matumizi sahihi ya bahari.

"Kuwa na mpango wa matumizi ya bahari ndipo utakapotambua uvuvi wa bahari kuu unaanzia wapi, uvuvi wa wavuvi wadogo na wakulima wa mwani," alieleza.

Alisema kukosekana kwa mpango huo kutakuwa na mwingiliano wa maeneo na ufanisi wa matumizi ya bahari hautopatikana na kufikia kuingia kwenye migogoro.

Alisema kuwapo kwao ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa malengo ya umoja wa mataifa katika ibara ya 14 ya maendeleo endelevu ambayo imesisitiza matumizi mazuri ya maeneo ya bahari. Alisema mpango wa matumiz

i ya bahari na uchumi wa buluu na mahitaji ya fedha ni jambo linalohitaji upeo mpana ili wawe na mpango mzuri wa bahari.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Aboud Suleiman Jumbe, alisema mpango huo umekuja kwa muda muafaka ambao serikali ina dhamira ya dhati ya kupanua wigo juu ya matumizi ya bahari.

Alisema mpango huo ni mpango tayarishi ambao utekelezaji wake ni muhimu katika maendeleo ya bahari.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Lucy Magembe, alisema uwapo wao ni kusaidiana na serikali mbalimbali katika dhana yao ya kuhifadhi mazingira ya bahari.

# Wavuvi wenye mgogoro watakiwa kuacha jazba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUFUATIA mgogoro kati ya wavuvi wa kijiji cha Uroa na Michamvi, Mkoa wa Kusini Unguja, serikali imewataka wavuvi wa pande mbili hizo kupunguza jazba na hasira kwa sababu tatizo hilo linafanyiwa kazi ili suluhu ipatikane.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Idara ya Uhifadhi wa Bahari, Dk. Makame Omar Makame, wakati akipozungumza na waandishi wa habari kufuatia kuwepo malalamiko ya wavuvi wa Uroa ambao wanadai kuzuiliwa kuitumia bahari katika eneo la bahari ya Uroa iliyopakana na Michamvi kwa ajili ya uvuvi.

Alisema wizara kupitia idara zake mbili baada ya kujitokeza sintofahamu hiyo ilikaa vikao na kamati zote kutafuta suluhu ili mgogoro huo usiendelee.

"Kuhusu kinachoendelea baina ya Michamvi na Uroa na jamii inayozunguka katika eneo hili, hilo tunalielewa na kama wizara na idara zetu mbili ya uvuvi na hifadhi tumeshakaa vikao na kamati zote mbili kuwashajiisha wajizuie na hayo madai yao yanafanyiwa kazi," alisema.

Alisema, kimtazamo mgogoro huo una njia mbili kutokana na madai ya wavuvi wa Uroa kwamba hata kama ufugaji wa pweza haupo, lakini wanapokwenda Michamvi wanazuiliwa.

"Katika kikao ambacho tuliwakutanisha kamati zote mbili tuliwaambia sisi kama serikali bahari yetu haina mipaka kila mtu anavua popote ili mradi havunji utaratibu kwani uvuvi una utaratibu zake, na uvuvi usiokuwa na utaratibu haukubaliki popote pale," alisema.

Hata hivyo, alisema wanalifuatilia kwa kina suala hilo ili kujua kiini cha mgogoro huo kutokana na kile ambacho alidai huenda kukawa kuna uvuvi haramu unafanyika.

Alisema katika kila shehia kuna kamati za kupambana na uvuvi haramu, lakini wanawashajiisha wasitumie nguvu katika kukabiliana na wavuvi ambao wanatumia utaratibu usiokubalika.

Wakizungumzia mgogoro huo wananchi na wavuvi wa kijiji cha Uroa walisema wao hawana wasiwasi na serikali ila wanachokitaka ni kuona haki inatendeka kwa pande zote mbili.

Ali Ibrahim Ali, ni miongoni mwa wavuvi wa kijiji hicho, alisema kijiji chao kimekuwa na eneo kubwa la uvuvi ambalo hutumiwa na wavuvi wote waliopo katika wilaya yao, kilichotokezea ni kila mtu kufunga eneo lake jambo ambalo limesababisha kudumaza maendeleo ya uvuvi.

"Sisi tunachokishangaa ni kuona kama hapa kuna kitu ndani yake kutokana na kwamba licha ya serikali kusema bahari haina mipaka, lakini wao wanapokwenda kuvua wanakatazwa," alisema Ibrahim.

Alisema wanachokitaka wavuvi wa Uroa kwa serikali ni kuwa na bahari huru isipokuwa mtu afuate utaratibu wa kisheria za kivuvi.

Naye mvuvi, Nyejua Khamis Suleiman, alisema bahari ambayo wanaitumia ni ya wana vijiji wote awe katoka Michamvi, Uroa, Pongwe na vijiji vingine, ambao wote ni damu moja na kitendo cha kutakiwa kuvua kijiji kimoja na wao kukatazwa sio haki na kuendelea kwake kutasababisha migogoro na uvunjifu wa amani.

# Watakiwa kutokuwa chanzo cha kukwamisha sensa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAUMINI wa dini ya Kiislamu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kutokuwa chanzo cha kukwamisha zoezi la sensa ya watu na makazi litakapoanza na badala yake wajitokeze kwa wingi kama wanavyojitokeza wakati wa ufunguzi wa misikiti sehemu mbalimbali.

Sensa ya watu na makazi inatarajia kuanza Agosti 23, mwaka huu, kwa kupitia nyumba hadi nyumba nchini nzima.

Hayo yalibainishwa jana na Sheikh wa Wilaya Al-Haji Omary Damka wakati wa zoezi la ufunguzi wa Msikiti wa Jamiu Hamza Bin Abdulmutwakib(R.A) katika kata ya Mungula Manispaa ya Kahama uliojengwa kwa hisani ya watu wafanyao heri kutoka nchini Oman chini ya Jumuiya ya International Istiqaama.

Alisema, itakuwa jambo la ajabu kama atasikia au kubaini kuna waumini wa dini ya kiislamu wanapinga na kuhamasisha watu wasishiriki zoezi la sensa ya watu na makazi na kwamba uwepo wa zoezi hilo ulianza tangu kwa mitume wa Mungu waliotangulia hivyo sio jambo jipya.

Damka alisema, hata kabla ya kujenga nyumba za ibada (Misikiti) sehemu mbalimbali hapa nchini wanafanya kwanza sensa ya kujua idadi ya waumini wa kiislamu waliopo eneo panapotakiwa kujenga, hivyo hatasijikia vema pale waumini watakapotajwa kuwa sehemu ya kukwamisha zoezi.

"Sisi katika zoezi hili tunatakiwa kuwa mfano wa kuigwa, tujitokeze kwa wingi na kushiriki zoezi hili na atakayebainika kukwamisha atakuwa ameichafua dini yetu na sisi hatutaweza kumvumilia kwa sababu jambo hilo lipo kisheria na sio jipya maskioni mwetu," alisema Damka.

Hata hivyo Damka aliwataka pia kutowaficha watoto wao wenye ulemavu mbalimbali wakati wa zoezi hilo kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na haki za binadamu, unaweza kushtakiwa na mbele za Mungu ni kosa kumnyima mtu kutambulika na serikali yake kwa ajili ya maandalizi ya maendeleo.

Mmoja wa waumini wa dini hiyo Athumani Miraji alisema, atahakikisha katika eneo lake analotoka anakuwa miongoni mwa wahamasishaji wazuri wa zoezi la sensa ili kuhakikisha wote wanashiriki bila kubagua itakadi za dini walizonazo.




Mkuu wa Huduma za Rejareja wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo, akizungumza na wateja wa benki hiyo mkoani Mwanza, katika hafla ya chakula maalum kwa ajili ya wateja, iliyolenga kutoa wasaa wa kujadili fursa za biashara, mipango ya ukuaji na huduma zitolewazo na benki hiyo katika mkoa huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Elimu ya unywaji kistarabu kwa mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imezindua tovuti inayotoa elimu juu ya unywaji pombe wa kistaarabu, ikiwa ni sehemu ya kusaidia umma kuwa na uelewa mpana zaidi juu ya matumizi ya pombe.

Tovuti hiyo inayojulikana kama DRINKiQ, ipo katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza, inaweza kutumiwa na mtu yeyote popote pale alipo bila malipo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma SBL, John Wanyancha, tovuti ya DRINKiQ imebeba taarifa mbalimbali ikiwa ni namna ambavyo pombe inaweza kuathiria mwili, namna ambavyo pombe inaingia mwilini na kuathiri uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi na kipimo cha kilevi katika vinywaji tofauti kama bia, pombe kali na nyinginezo.

"DRINKiQ ni sehemu muhimu ya mkakati wa SBL ya kuwasaidia watumiaji wa bidhaa zake na umma kwa ujumla kufanya maamuzi sahihi juu ya unywaji pombe," anasema Wanyancha.

Anaongeza: "Tunayo furaha kuona namna ambavyo mafunzo kupitia DRINKiQ yamepokelewa na umma wa Watanzania katika miaka michache ambayo tumekuwa tukiyatoa. Huu ni ushahidi tosha kuwa wanywaji walikuwa na kiu ya kupata aina hii ya elimu na kupitia namna mpya ya utolewaji kwa njia ya mtandao ni wazi kuwa Watanzania wengi zaidi popote pale walipo wataweza kunufaika.

Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa kwa wale ambao wamechagua kunywa pombe, DRINKiQ, itawasaidia kufahamu kiasi cha kilevi kilichopo katika pombe za aina mbali mbali ambazo wanatumia au wangependa kutumia. DRINKiQ ni chombo muhimu ambacho kitamsaidia mnywaji kujua kilichopo kwenye kinywaji anachotumia na hivyo kuweka kikomo cha nini atumie na kwa muda gani.

Wwanyancha alisema wakati baadhi ya watu wakichagua kunywa kistarabu, wengine wengi hawafanyi hivyo na kuongeza kuwa kampuni ya SBL imekuwa na itaendelea kuwa mstari wa mbele kutoa elimu juu ya unywaji wa kistarabu kwa njia mbali mbali ikiwamo kwa njia ya mtandao.

Taasisi ya Afya na Uzalishaji ya Marekani imeunga mkono mafunzo kwa njia ya mtandao juu ya unywaji wa kistarabu kupitia DRINKiQ na kusema kuwa utaratibu unatumika ni rahisi kwa mtu yeyote kujifunza na pia utaongeza uelewa juu ya athari za unywaji usio wa kistarabu na pia utasaidia kuongoza matumizi ya kistaarabu ya pombe.

# Kanda ya Ziwa kunufaika zaidi huduma za kibenki

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Kanda ya Ziwa wamehakikishiwa huduma zaidi za kibenki kwa kiongezewa matawi na mawakala.

Mkoa wa Mwanza umetajwa kuwa utanufaidika zaidi baada ya Benki ya Exim Tanzania kuombwa kuangalia namna ya kujitanua zaidi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa hususani katika mkoa wa Mwanza kwa kufungua matawi zaidi sambamba na huduma za uwakala ili iweze kuwafikia wateja wengi zaidi katika ukanda huo wanaohitaji huduma za kifedha kutoka benki hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, wakati wa hafla ya chakula maalum kwa ajili ya wateja wa benki hiyo mkoani Mwanza mwishoni mwa wiki Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Kanali Denis Filangali Mwila, pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa huduma zake bora mkoani humo aliuomba uongozi wa benki hiyo kuangalia namna ya kujitanua zaidi mkoani humo kwa kuongeza matawi zaidi kwenye wilaya mbalimbali za mkoa huo ili huduma zake ziweze kuwanufaisha wananchi wengi wa mkoa huo.

"Katika kipindi chote cha uwepo wake hapa jijini Mwanza Benki ya Exim imekuwa na mchango mkubwa kwa wakazi wa mkoa huu kwa kutoa huduma zinazowalenga haswa wakazi wa hapa ikiwamo mikopo ya biashara, mikopo ya watumishi na sasa mmekuja na huduma mahususi kwa ajili ya wajasirimali. Nashauri sasa muone umuhimu wa kujitanua zaidi katika mkoa huu na ukanda wote wa Ziwa ili wananchi wafikiwe na huduma hizi nzuri," alisema Kanali Mwila.

Kanali Mwila alisema mchango wa benki hiyo mkoani humo haujaishia katika utoaji wa huduma za kifedha tu bali pia imekuwa mdau muhimu wa maendeleo ya mkoa kupitia mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii.

"Ni hivi karibuni tu tulipokea madawati takribani 100 kutoka Benki ya Exim na bado benki hii imeendelea kufungua milango yake ya kushirikiana na serikali katika kufanikisha mipango mingine mingi ya kimaendeleo. Ni kutokana na sababu kama hizi ndio maana nasi tunawaunga mkono kwa kuwahamasisha wananchi kujiunga na huduma zenu," alisema.

Awali akizungumza kwenye hafla iliyohudhuliwa na wadau mbalimbali wa benki hiyo wakiwamo viongozi wa kiserikali, wafanyabiashara wakubwa na wadogo pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo ikilenga kutoa wasaa wa kujadili fursa za kibiashara, mipango ya ukuaji na huduma zitolewazo na benki hiyo katika mkoa huo, Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo, alisema benki hiyo imejipanga zaidi kwa kuboresha mifumo na taratibu za utoaji huduma ili ziendane na mahitaji halisi ya wateja na soko.

TANGAZO

Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MARCH 2022.
Kiwango kwa Tzs.

| | | Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-22 TZS | Robo Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 773,400,659 | 811,284,530 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 35,945,090 | 99,362,319 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 52,610,075 | 27,602,387 |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | | |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 12,902,347,747 | 13,801,091,769 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,226,572,757 | 1,458,387,098 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 | Akaunti za udhamini | | |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,375,912,197 | 1,773,501,419 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **17,366,788,526** | **17,971,229,522** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 | Amana za Wateja | 2,618,645,637 | 2,274,439,496 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 | Amana Maalumu | 1,284,601,479 | 1,418,407,594 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | | |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | | |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi | | |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 379,129,895 | 277,852,173 |
| 28 | Madeni | 6,103,965,000 | 5,650,000,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **10,386,342,011** | **9,620,996,263** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **6,980,446,515** | **8,350,233,259** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 6,056,496,547 | 6,056,496,547 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | | |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | 1,226,400,000 | 2,439,473,000 |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | (354,922,914) | -207,854,619 |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | 52,472,881 | 62,118,331 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **6,980,446,515** | **8,350,223,259** |
| | | **17,366,788,526** | **17,971,229,522** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | | |
| 39 | Mikopo chechefu | 3,812,399,297 | 3,194,085,725 |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | 1,081,983,192 | 605,675,243 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | % | % |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 40% | 46% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo | 18% | 23% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 358% | 390% |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 74% | 77% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81% | 80% |
| vi | Ongezeko la Amana | 15% | 1% |
| vii | Ongezeko la Mali | -3% | -2% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 MARCH 2022.
Kiwango kwa Tzs.'(000)'

| | Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-22 TZS | Robo Mwaka Uliopita 31-Dec-21 TZS | imbikizo Robo Mwak wa sasa 31-Mar-22 TZS |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 937,819,062 | 1,072,410,349 | 937,819,062 |
| Gharama za Riba | 140,214,637 | 109,311,397 | 140,214,637 |
| **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **797,604,425** | **963,098,953** | **797,604,425** |
| Madeni Viza Yaliyofutwa | | | |
| Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | 80,351,672 | -27,793,822 | 80,351,672 |
| **Mapato yasiyo ya Riba:** | **142,982,631** | **151,597,635** | **142,982,631** |
| 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 90,805,373 | 110,717,422 | 90,805,373 |
| 6.3 Gawio | | | |
| 6.4 Mapato Mengine | 52,177,258 | 40,880,213 | 52,177,258 |
| **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,215,158,298** | **1,439,425,580** | **1,215,158,298** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 587,707,299 | 636,722,799 | 587,707,299 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 6,605,205 | 36436487.32 | 6,605,205 |
| 7.3 Gharama nyingine | 620,845,793 | 766,266,294 | 620,845,793 |
| **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **(354,922,914)** | **(296,935,170)** | **(354,922,914)** |
| Tengo la Kodi ya Mapato | - | (89,080,551) | |
| **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **(354,922,914)** | **(207,854,619)** | **(354,922,914)** |
| Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | | | |
| **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **(354,922,914)** | **(207,854,619)** | **(354,922,914)** |
| Idadi ya Waajiriwa | 127 | 129 | 127 |
| Mapato kwa Hisa | -29 | 13 | -29 |
| Idadi ya Matawi | 3 | 3 | 3 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2% | -1% | -2% |
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa | -5% | -2% | -5% |
| Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 66% | 71% | 66% |
| Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6% | 7% | 6% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MARCH 2022
Kiwango kwa Tzs '(000)'

| | | Robo Mwaka wa sasa 31-Mar-22 TZS | Robo Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **(354,922,914)** | **(207,854,619)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | | |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **80,351,672** | **101,590,391** |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | - | - |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | | |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | | **(274,571,242)** | **(106,264,229)** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | | |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | 898,744,022 | 743,323,600 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (768,185,660) | (76,724,056) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 344,206,141 | 119,792,964 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | (134,103,115) | (645,659,000) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 101,277,722 | 48,015,580 |
| | | **167,367,868** | **82,484,859** |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | (89,080,551) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **167,367,868** | **(6,595,692)** |
| | | - | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (98,649,431) | 62,372,122 |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | Mengineyo Amana za kudumu | - | - |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa*** | **(98,649,431)** | **62,372,122** |
| | | - | **0%** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | (100,000,000) | (50,000,000) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (45,011,850) | (46,495,249) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | | |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **(145,011,850)** | **(96,495,249)** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha | **(76,293,413)** | **(40,718,818)** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | **938,249,237** | **978,968,055** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **861,955,825** | **938,249,237** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MARCH 2022

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa Hisa | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | Akaunti zingine za Mtaji | | Tengo la ziada ya juma | | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Salio la wa mwaka 01/01/2021 | 6,056,497 | - | - | 69,693 | | 2,332,349 | | 8,458,539 |
| Rekebisho : | | | | | | | | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | - | (7,574) | | - | | (7,574) |
| Mapato mengine | | | | | | | | - |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | | - | | | - | | - |
| Tozo la Mali la mwaka jana | - | - | - | | | 434,618 | | 434,618 |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | | | (262,797) | | (262,797) |
| Gawio lililolipwa | | | | | | (272,551) | | (272,551) |
| **Salio kwa Mwaka 31.12.2021** | **6,056,497** | **-** | **-** | **62,118** | | **2,231,618** | | **8,350,233** |
| **Salio la mwaka 01.01.2022** | **6,056,497** | **-** | **-** | **62,118** | | **1,226,400** | **#** | **7,345,015** |
| Rekebisho : | - | | | | | | | - |
| Akaunti zingine za Mtaji | - | | | (9,645) | | | | (9,645) |
| Toa: Mapato mengine | - | | | | | | | - |
| Mtaji wa kisheria | - | | - | | | | | - |
| | - | | | | | 0 | | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | | (354,922) | | (354,922) |
| Toa: Gawio lililotolewa | - | | | | | - | | - |
| **Salio kwa mwaka 31.03.2022** | **6,056,497** | **-** | **-** | **52,473** | | **871,478** | **#** | **6,980,448** |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.03.2022

AINA YA BIDHAA

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | 2. MIKOPO | | |
|---|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufungua akaunti | 5000/= | Mikopo ya biashara | | 36% PA |
| Ada ya mwezi | BURE | Mikopo ya kuboresha nyumba | | 18% PA |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | Ada ya Mkopo | | 2.50% |
| Kuuliza salio | BURE | Bima ya mkopo | | 2.00% |
| Kufunga akaunti | 5000/= | Mikopo ya Jikimu | | 17% PA |
| Gharama za kuendesha akaunti | 5000/= | Mikopo ya Kilimo | | 30% PA |
| Gharama za kuweka fedha | BURE | Mikopo ya Maji | | 26% PA |
| | | Mikopo ya wafanyakazi | | 15% PA |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| **Imesainiwa na:** | **Cheo** | | **Tarehe:** |
|---|---|---|---|
| *Altemius Millinga* | *Mkurugenzi Mtendaji* | .............................. | *16-Mei-22* |
| *Theresiah Chimbwi* | *Kaimu Meneja wa Fedha* | .............................. | *16-Mei-22* |
| *Humphrey Singogo* | *Kaimu Mkaguzi wa Ndani* | .............................. | *16-Mei-22* |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Kuthibitishwa na:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Ernest K. Ndimbo* | *Mwenyekiti wa Bodi* | .............................. | *16-Mei-22* |
| *Happy Sambega* | *Mkurugenzi* | .............................. | *16-Mei-22* |

# MAKATA, MENEJA WAOMBA RADHI 'JELA' YA SOKA MIAKA 5

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu na Meneja wa timu ya Mbeya Kwanza, Mbwana Makata na David Naftar, wameomba radhi Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kwa kosa walilodaiwa kufanya la kuwashawishi wachezaji wao kugomea mechi dhidi ya Namungo FC, hivyo kusababishia wawili hao kufungiwa kujihusisha na soka kwa miaka mitano.

**Wakizungumza na gazeti hili jana, Kocha Makata alisema tayari wameandika barua ya kuomba kupitiwa upya kwa hukumu yao katika kamati husika.**

Lakini pia alisema wameomba radhi TFF na Bodi ya Ligi pamoja na wadau wa soka kwa kitendo kilichotokea kwa kuwa hakikuwa kizuri kwa maendeleo ya soka, hivyo wanajutia kosa walilofanya.

"Ligi yetu ina mafanikio makubwa, hatutakiwi kuwa watu wa kuitia doa, najutia kwa kitendo nilichokifanya na kuahidi kutorudia tena hapo nitakapofunguliwa na kusamehewa adhabu yangu," alisema Makata.

Alisema hawajakata rufani ila wamepeleka maombi yao kwa kamati husika kuhakikisha wanapitia upya adhabu yao na kuomba kufutiwa.

Kwa upande wa Meneja wa timu hiyo, Naftal alisema anajutia kitendo alichokifanya katika mchezo wao dhidi ya Namungo FC na kusababishwa kupewa adhabu kubwa ya kufungiwa miaka mitano.

"Sitakuwa tofauti na Kocha Makata, binafsi najutia kwa hali iliyosababisha hadi kuadhibiwa na kamati husika, naomba msamaha kwa TFF, Bodi na wadau wa soka kwa kitendo nilichokifanya katika mchezo wetu dhidi ya Namungo," alisema Naftali.

Makata na Naftali wamefungiwa kwa kipindi cha miaka mitano kila mmoja kwa kosa la kushawishi/kuamuru wachezaji wasiingie uwanjani kuanza mchezo kati ya Namungo dhidi ya Mbeya Kwanza kutokana na gari la kubebea wagonjwa/majeruhi kutokuwapo uwanjani siku ya mchezo huo mjini Lindi, hata lilipokuja walidai ilikuwa nje ya muda, hivyo kuamuru wachezaji wao kuondoka uwanjani.

Tukio hilo lilisababisha mchezo usifanyike na kuchafua taswira ya ligi ikiwamo kusababisha hasara kwa wadhamini wa Ligi Kuu baada ya Mbeya Kwanza kugoma kucheza kwa kile walichoeleza kuwa ni kutokamilika kwa moja ya taratibu za maandalizi ya mchezo.

# *Baseball kuivaa Misri na uzi mpya*

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Chama cha Mchezo wa Baseball na Softball Tanzania (TaBSA), umezindua jezi ya timu ya taifa ya mchezo huo ambayo leo inashuka dimbani kupambana na Misri katika mashindano ya BaseBall 5 Afrika yanayoanza kutimua vumbi Dar es Salaam leo hadi Ijumaa wiki hii.

Akizungumza jijini jana baada ya uzinduzi huo, Katibu Mkuu wa chama hicho, Alpherio Nchimbi, alisema anashukuru wamefanikiwa kuzindua jezi hiyo yenye lengo la kuitangaza nchi ya Tanzania kupitia mashindano hayo.

Alisema lengo la mashindano hayo ni kupata timu mbili ambazo zitashiriki mashindano ya Kombe la Dunia Novemba mwaka huu nchini Mexico.

Alisema mpaka timu zote zilizothibitisha kushiriki mashindano hayo, tayari zimewasili nchini kasoro Zimbabwe, Misri pamoja na Zambia ambazo zilitarajiwa kutua jana.

Alitaja nchi ambazo zitashiriki mashindano hayo kuwa ni Tunisia, Burkina Faso, Ghana, Uganda, Kenya, Afrika Kusini pamoja na wenyeji Tanzania. Alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamiilika na kwa upande wao hawana wasiwasi kwani timu yao imekaa kambini kwa muda mrefu ikijiandaa.

"Maandalizi yetu yamekamilika, timu yetu imekaa kambini kipindi kirefu, hivyo tunaamini tutafanya vizuri, tunaomba Watanzania waje kwa wingi uwanjani kushuhudia vipaji vinavyoonyeshwa na wachezaji wetu," alisema Nchimbi.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Maclina Mutabuzi, alisema wamejipanga vizuri kukutana na Wamisri hao kutokana na maandalizi waliyoyafanya.

"Tumejipanga vizuri kwani tumekaa kambini kipindi kirefu ambacho kimewasaidia kwa kiasi kikubwa wachezaji na leo (jana), tutafanya mazoezi ya mwisho jioni," alisema Mutabuzi.

## KIKAPU...



Mchezaji wa timu ya mpira wa Kikapu ya Unimatched, Kye Mwakalago, akiwatoka wachezaji wa timu ya Highview, katika michuano ya Jr. NBA at JKM Park, inayoendelea katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Katwila njiapanda Ihefu akiipa ubingwa

**Na Cheji Bakari, Tanga**

LICHA ya kuipandisha Ligi Kuu Bara na kuipa ubingwa wa Championship, Kocha Mkuu wa Ihefu FC ya jijini Mbeya, Zuberi Katwila (pichani), bado hajawa na uhakika wa kukinoa kikosi kuelekea msimu ujao wa ligi hiyo nchini, ameeleza.

Jumamosi Ihefu FC ilitwaa ubingwa wa Ligi ya Champioship baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ndanda FC katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona huku DTB iliyoongoza msimamo wa ligi hiyo kwa kipindi kirefu, ikichapwa bao 1-0 na Kitayosce kwenye mechi za kuhitimisha msimu wa ligi hiyo juzi, na zote mbili kumalizika na pointi 66, lakini kikosi hicho cha Katwila kikiwa na mabao mengi ya kufunga.

Ihefu ilipindua meza kibabe na kukaa kileleni kwenye mechi ya mwisho kutokana na kufunga mabao 50, huku DTB ikiwa na mabao 44.

Hata hivyo, Katwila ambaye alianza kuinoa timu hiyo katikati ya msimu wa Ligi Kuu 2020/21 wakati huo ikiwa katika mstari wa kushuka daraja, mwishoni mwa msimu huo alishuka nayo na sasa ameirejesha Ligi Kuu ikiwa ni pamoja na kuipa ubingwa wa Championship, lakini mkataba wa kocha huyo sasa umemalizika.



Akiungumza na mwandishi wetu kwa njia ya simu, Katwila alisema yupo tayari kuendelea kuitumikia timu hiyo kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu 2022/23 endapo wataingia makubaliano ya mkataba mpya na uongozi wa timu hiyo.

Ihefu FC na DTB FC zote zimejihakikishia kupanda Ligi Kuu msimu ujao.

Katwila alisema alikuwa na mkataba wa mwaka mmoja wa kuifundisha timu hiyo katika Ligi ya Championship, ambao sasa umemalizika, lakini yupo tayari kuendelea kuifundisha kama watafikia makubaliano na uongozi wa klabu hiyo.

"Ndio tumemaliza Ligi ya Championship leo (juzi), bado hatujakaa na uongozi, kwa hiyo siwezi kusema chochote, kama ikiwa tutakaa mezani na uongozi, tukakubaliana kuongeza mkataba, basi nitakuwa tayari," alisema.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POGBA AWA LULU

KLABU ya Paris St-Germain inaanda ofa ya mwisho kwa ajili ya Paul Pogba, 29, lakini Juventus wanajiamini kwamba, kiungo huyo Mfaransa mwenye miaka 29 atajiunga na timu hiyo kwa mkàtaba wenye thamani ya karibu pauni milioni 10 kwa msimu pale atakapomaliza mkataba wake Manchester United mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

### OSIMHEN AOTA MBAYA

OFA ya Arsenal ya pauni milioni 76 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23, imekataliwa na Napoli. ***(Calciomercato)***

### BROJA KUNG'OLEWA CHELSEA

KLABU za Newcastle, West Ham na Southampton zinamwania Armando Broja wa Chelsea. Raia huyo wa Albania mwenye miaka 20, anasakwa pia na Klabu za Italia, AC Milan, Inter Milan na Napoli. ***(Goal)***

### XAVI NA LEWANDOWSKI

KOCHA wa Barcelona, Xavi amethibitisha kwamba, wako kwenye mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33. ***(Goal)***

### KOSTIC KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur walipeleka wasaka vipaji wake kumwangalia winga wa Serbia, Filip Kostic akiisaidia Eintracht Frankfurt kutwaa taji la Ligi ya Europa wiki hii, na kwa sasa Spurs wanajiandaa kumsajili nyota huyo mwenye miaka 29, mwishoni mwa msimu kwa ada ya pauni milioni 25. ***(Express)***

### MANE HAONGEZWI MSHAHARA

LIVERPOOL watamwongezea mkataba, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, lakini hawana mpango wa kumwongezea mshahara mnono zaidi mshambuliaji huyo wa Senegal, ambaye amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa. ***(Football Insider)***

### TUCHEL KUSAJILI STRAIKA

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, atatafuta suluhu ya tatizo la ufungaji kwa timu yake kwa kusajili mshambuliaji mpya. ***(Guardian)***

### MATIC NA FULHAM

KLABU ya Fulham iliyopanda daraja msimu huu, inataka kuzungumza na kiungo wa Serbia, Nemanja Matic mwenye umri wa miaka 33, ili kumbakisha Ligi Kuu England baada ya kumalizana na Manchester United mwishoni mwa msimu. ***(Sun)***

### STRAKOSHA HUYOOO EPL

FULHAM pia wanakaribia kumsajili kipa wa Albania, Thomas Strakosha mwenye umri wa miaka 27 kutoka Lazio. ***(Gianluca di Marzio)***

### ISCO KUONDOKA MADRID

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amesema kiungo wa zamani wa Hispania, Isco mwenye umri wa miaka 30, ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu mkataba wake utakapomalizika. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AELEZEA FURAHA YAKE KUSAINI TENA PSG

●●● Nina furaha sana kuendelea kucheza hapa Paris Saint-Germain, kubaki Paris, jiji langu...

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe aliwahutubia mashabiki wa Paris Saint-Germain pale Parc des Princes kabla ya timu yake kukutana na Metz kwenye mechi ya mwisho ya Ligue 1 Jumamosi baada ya mshambuliaji huyo kusaini mkataba mpya na klabu hiyo.

**Mbele ya watu 47,000 walihudhuria, Mbappe alithibitisha kuwa ana furaha kusaini mkataba mpya na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.**

Mshambuliaji huyo, baada ya kushikilia jezi ya 'Mbappe 2025' ya PSG, alisema: "Nina furaha sana kuendelea kucheza hapa Paris Saint-Germain. Kubaki Paris, jiji langu.

"Natumaini nitaendelea kufanya kile ninachopendelea nikiwa nanyi nyote...na kushinda mataji pamoja! Asante sana".

Kwa muda mrefu Mbappe alitarajiwa kuhamia Real Madrid kama mchezaji huru msimu huu wa majira ya joto, baada ya kuwindwa na 'Los Blancos' hao kwa miaka kadhaa. Lakini katika hali isiyotarajiwa nyota huyo wa Ufaransa sasa ameweka mustakabali wake kwa PSG hadi mwaka 2025.

Mshambuliaji huyo amefurahia msimu mzuri wa 2021/22 pale PSG, akishinda kuwa mchezaji bora wa Ligue 1 kwa mara ya tatu na kufunga mabao 25 ya kuvutia kwenye ligi.

Sasa Mbappe atakuwa na matumaini kuwa anaweza kuiongoza PSG kupata mafanikio zaidi, haswa barani Ulaya ambapo klabu hiyo imekuwa ikishindwa kuwika.

Awali, PSG ilithibitisha kuwa Mbappe amesaini mkataba mpya na klabu hiyo.

Mkataba wa awali wa Mfaransa huyo ulikuwa unamalizika msimu huu wa majira ya joto na alionekana kama ataondoka.

'Los Blancos' walikuwa na imani kwamba dili kubwa la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, limekubaliwa, lakini imani ya PSG kwamba Mbappe, angesalia Parc des Princes iliongezeka katika siku za hivi karibuni.

Na mabingwa hao wa Ligue 1 walithibitisha Jumamosi kwamba Mbappe amesaini mkataba mpya katika mji mkuu wa Ufaransa ambao utadumu hadi mwaka 2025.

Mbappe amebakisha mabao 32 ili kuwa mfungaji bora wa muda wote wa PSG na ana nafasi kubwa ya kumpita Edinson Cavani msimu ujao kama mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
DODOMA FC
VERSUS
NAMUNGO
1 | 2.48
X | 2.63
2 | 3.16

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE BRUYNE, FODEN WACHEZAJI BORA EPL MSIMU WA 2021-22



**LONDON,** England

KEVIN de Bruyne wa Manchester City amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa msimu wa 2021-22 wa Ligi Kuu ya England, huku mchezaji mwenzake, Phil Foden akichaguliwa kuwa mchezaji bora chipukizi.

Kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji, De Bruyne, amefunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho saba, huku City wakiwa kileleni mwa ligi kabla ya siku ya mwisho ya msimu, jana Jumapili.


"Kushinda tuzo hii kwa mara ya pili ni mafanikio ambayo ninajivunia sana," alisema De Bruyne akiwaambia waandishi wa habari.

De Bruyne mwenye miaka 30, alichaguliwa baada ya kura kutoka kwa umma kwenye tovuti ya Ligi Kuu England na kuunganishwa na zile za manahodha 20 wa klabu za ligi hiyo na jopo la wataalamu wa soka.

Bruyne aliwashinda, mwenzake wa City, Joao Cancelo na wawili wa Liverpool, Mohamed Salah na Trent Alexander-Arnold, Jarrod Bowen wa West Ham, Bukayo Saka wa Arsenal, mshambuliaji wa Tottenham, Son Heung-min na kiungo wa kati wa Southampton, James Ward-Prowse.

De Bruyne pia alidai tuzo hiyo inamfanya aungane na Thierry Henry, Cristiano Ronaldo na Nemanja Vidic kushinda zaidi ya mara moja.

"Kuna ubora mwingi kwenye Ligi Kuu, ni furaha kuteuliwa na wachezaji wengine wengi wazuri ambao wamekuwa na msimu ya kuvutia kwenye klabu zao," alionGeza De Bruyne.



## *Mata: Asiye na viwango hapaswi kuwa Manchester United*

**MANCHESTER,** England

JUAN Mata ametoa wito kwamba, mchezaji yeyote ambaye hafikii viwango ndani ya Manchester United hapaswi kuwa hapo Old Trafford.

United wamekuwa na msimu mwingine mbaya na bila kujali matokeo katika mchezo wao wa mwisho wa jana Jumapili dhidi ya Crystal Palace, watamaliza wakiwa na pointi zao za chini zaidi katika historia ya Ligi Kuu England.

Ole Gunnar Solskjaer alifutwa kazi mwishoni mwa Novemba kabla ya uteuzi wa muda mfupi wa Ralf Rangnick, ambaye ataondoka akiwa na kiwango cha chini zaidi cha ushindi kuliko kocha yeyote wa United katika historia ya Ligi Kuu (asilimia 43.5, ushindi 10 katika mechi 23).

Erik ten Hag ndiye kocha anayefuata aliyepewa jukumu la kubadilisha hali pale United, na kiungo Mata alihimiza maboresho kwa kikosi hicho msimu ujao.

"Ni wazi kuwa uwanjani, tumefanya makosa mengi," alisema Mata akiiambia The Athletic.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# SONGO AMFUNIKA TAMBWE UFUNGAJI BORA CHAMPIONSHIP

**Na Cheji Bakari,** Tanga

WAKATI msimu wa Ligi ya Championship 2021/22 ukimalizika juzi, Jumamosi kwa Ihefu FC jijini Mbeya kutwaa ubingwa ikiwa ni pamoja na kuungana na DTB FC ya Dar es Salaam kupanda Ligi Ligi Kuu Bara kwa msimu ujao, mshambuliaji wa JKT Tanzania, Edward Songo ameibuka mfungaji bora.

Jumamosi Ihefu FC ilitwaa ubingwa wa ligi hiyo baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ndanda FC katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona huku DTB iliyoongoza msimamo wa Championship kwa kipindi kirefu, ikichapwa bao 1-0 na Kitayosce kwenye mechi za kuhitimisha msimu.

**Matokeo hayo yanazifanya timu hizo, zote kuhitimisha msimu zikiwa na pointi 66, lakini Ihefu ikiwa na mabao 50 ya kufunga dhidi ya 44 ya DTB.**

Hata hivyo, kwa upande wa mbio za Kiatu cha Dhahabu kwa mfungaji bora wa ligi hiyo, Straika wa JKT Tanzania, Songo amempiku Amissi Tambwe wa DTB FC, ambaye alikuwa akipewa nafasi kubwa ya kuibuka mfungaji bora kutokana na kasi yake ya kucheka na nyavu.

Songo amemaliza msimu na akiwa na mabao 15, moja zaidi ya Tambwe, huku Danny Mrwanda wa KenGold akihitimisha na mabao 13 katika nafasi ya tatu akifuatiwa na Nicholas Gyan wa DTB FC mwenye mabao 12.

Wachezaji wengine walioonyesha uwezo wa kucheka na nyavu katika ligi hiyo ni Andrea Sinchimba wa Ihefu FC, ambaye amemaliza na mabao 11, Abiud Mtambula wa Kitayosce FC mabao tisa sawa na Mohamed Hamisi wa Mashujaa FC na Warsha Machungwa wa Mwadui FC.

Kitayosce FC ya mkoani Tabora iliyomaliza ligi hiyo ikiwa nafasi ya tatu baada ya kujikusanyia jumla ya alama 61 JKT Tanzania iliyoshika nafasi ya nne kutokana na pointi zake 51, zitacheza mechi ya mchujo (play-off) na timu itakayoshinda itakutana na ya mshindi wa play-off kutoka Ligi Kuu kuwania kucheza ligi hiyo msimu ujao.

# Azam hesabu sasa kwa Ruvu Shooting



**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Mtibwa Sugar, Azam FC imesema mkakati wao sasa ni kuzisaka pointi tatu katika mchezo wao ujao wa Ligi Kuu dhidi ya Ruvu Shooting kesho, Jumanne.

Mtibwa Sugar ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Manungu Complex juzi, ilikubali kipigo hicho kutoka kwa Azam FC ambacho sasa kinaiweka katika nafasi ya nne ikiwa na alama 36, moja nyuma ya Namungo FC iliyopo nafasi ya tatu kabla ya mechi za jana. Mtibwa imebaki nafasi ya 10 na pointi zake 28.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa Azam FC, Thabit Zakaria 'Zaka Zakazi', alisema, Kocha wao Mkuu, Abdihamid Moallin, amesema matokeo hayo ni muhimu kwao na kuahidi kupambana akiwa na lengo la kushika nafasi ya juu.

"Tunashukuru tumepata pointi tatu katika mchezo huo kwa sasa tunajiandaa na mchezo wetu ujao dhidi ya timu ya Ruvu Shooting, tutakaoucheza Mei 24 (kesho)," alisema Zakazi.

Alisema wachezaji wanaendelea na mazoezi kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mchezo huo ambao anaamini utakuwa na ushindani mkubwa kutokana na timu nyingi kuanzia nafasi ya tatu kutofautiana ponti chache.

"Lengo ni kufanya vizuri katika michezo yetu iliyobaki ili kuhakikisha tunashikilia nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC msimu huu."

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 23/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5269 | Hadiya Hosahina FC vs Wolkite City FC | 2.38 | 2.68 | 3.26 |
| 13:30 | 2312 | Gorilla FC vs APR FC | 5.25 | 3.25 | 1.66 |
| 14:00 | 3053 | Kocaelispor U19 vs Istanbulspor U19 | 1.95 | 3.46 | 3.36 |
| 14:00 | 3623 | FC Yessentuki vs Chernomorets N. | 8.75 | 6.41 | 1.21 |
| 15:00 | 2065 | Senja FK vs Stromsgodset 2 | 4.19 | 4.39 | 1.58 |
| 16:00 | 1044 | FK Haugesund 2 vs Viking FK 2 | 8.94 | 6.61 | 1.20 |
| 16:00 | 4240 | Kiyovu Sports vs Etoile de Lest | 1.27 | 4.87 | 9.54 |
| 16:00 | 4274 | Mukura vs Gicumbi | 1.58 | 3.75 | 5.80 |
| 16:00 | 4819 | Mekelakeya vs Dire Dawa Kenema FC | 2.48 | 2.85 | 3.20 |
| 16:00 | 5257 | Odds BK 2 vs Sotra | 2.23 | 3.44 | 2.77 |
| 17:00 | 1235 | Dinamo Samarqand vs Otmk Olmaliq | 5.25 | 3.25 | 1.66 |
| 17:00 | 1336 | Qizilqum vs Surkhon Termez | 1.67 | 3.22 | 5.27 |
| 17:00 | 3400 | Lokomotiv Tashkent vs Pakhtakor | 4.37 | 3.45 | 1.72 |
| 17:00 | 3418 | Inter Luanda vs Sporting de Benguela | 1.34 | 4.80 | 8.60 |
| 17:00 | 3439 | P. Associacao Do Sambizanga vs CD Lunda Sul | 1.97 | 3.02 | 3.85 |
| 17:00 | 4741 | Sportive Zarzis vs Olympique de Beja | 2.95 | 2.60 | 2.85 |
| 17:00 | 5048 | Wiliete SC vs Kabuscorp Scp | 1.61 | 3.60 | 5.80 |
| 17:00 | 5759 | ES Hammam Sousse vs ES Metlaoui | 1.44 | 3.60 | 7.79 |
| 18:00 | 2303 | FK Panevezys B vs Vmfd Zalgiris-3 | 2.63 | 3.99 | 2.13 |
| 18:00 | 2956 | Hifk vs KuPS Kuopio | 6.24 | 3.90 | 1.46 |
| 18:00 | 3396 | Valerenga IF 2 vs Ullensaker/Kisa | 5.46 | 4.68 | 1.42 |
| 18:30 | 4346 | FS Metta/Lu vs FC Riga | 19.42 | 7.77 | 1.09 |
| 18:30 | 5756 | Randesund IL vs Sarpsborg Sparta 2 | 4.26 | 4.26 | 1.59 |
| 19:00 | 1001 | Ranheim vs IK Start | 3.12 | 3.65 | 1.98 |
| 19:00 | 1050 | Dodoma FC vs Namungo | 2.48 | 2.63 | 3.16 |
| 19:00 | 1572 | Kfum Oslo vs Kongsvinger IL | 2.06 | 3.46 | 3.07 |
| 19:00 | 2356 | Grorud IL vs Bryne | 2.06 | 3.46 | 3.07 |
| 19:00 | 3000 | Express IL vs Fredrikstad FK 2 | 3.36 | 4.58 | 1.71 |
| 19:00 | 3093 | Sandnes Ulf vs Mjondalen | 2.21 | 3.41 | 2.82 |
| 19:00 | 3611 | Viljandi Tulevik vs Harju JK Laagri | 8.61 | 6.21 | 1.26 |
| 19:00 | 5393 | Skeid Fotball vs Stjordals-Blink | 2.13 | 3.46 | 2.92 |
| 19:30 | 1299 | Farco FC vs El Gouna | 2.45 | 2.79 | 3.24 |
| 20:00 | 1946 | Nykobing FC vs Lyngby | 6.03 | 4.76 | 1.38 |
| 20:00 | 2390 | GIF Sundsvall vs Mjallby | 3.11 | 3.21 | 2.14 |
| 20:00 | 2583 | WSG Wattens vs LASK Linz | 3.60 | 3.99 | 1.75 |
| 20:00 | 3151 | Hvidovre IF vs FC Helsingor | 3.51 | 3.56 | 1.87 |
| 20:00 | 3184 | FC Fredericia vs Horsens | 3.65 | 3.74 | 1.79 |
| 20:00 | 3407 | Orebro SK vs AFC Eskilstuna | 1.82 | 3.73 | 4.14 |
| 20:00 | 5293 | Norrby IF vs Utsiktens BK | 1.79 | 3.69 | 4.35 |
| 20:00 | 5445 | Halmstads BK vs Brommapojkarna | 1.76 | 3.84 | 4.34 |
| 20:30 | 4355 | Argesul Pitesti vs Voluntari | 2.57 | 2.87 | 2.92 |
| 21:30 | 1725 | Hamburger SV vs Hertha BSC | 2.17 | 3.23 | 3.23 |
| 21:35 | 4342 | Deportivo Riestra vs Temperley | 2.13 | 2.77 | 3.70 |
| 21:45 | 2227 | Drogheda Utd vs Shamrock Rovers | 10.70 | 5.25 | 1.23 |
| 21:45 | 2609 | Shelbourne vs UCD Dublin | 1.50 | 3.84 | 5.83 |
| 21:45 | 2681 | Notts County vs Grimsby | 1.96 | 3.45 | 3.50 |
| 21:45 | 4126 | Sligo Rovers vs Derry City | 3.50 | 3.26 | 1.97 |
| 21:45 | 5701 | St Johnstone vs Inverness | 1.83 | 3.38 | 4.28 |
| 21:45 | 5750 | St Patricks vs Bohemians FC | 2.19 | 3.21 | 3.02 |
| 22:00 | 5699 | Finn Harps vs Dundalk FC | 3.70 | 3.31 | 1.90 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Mei 23, 2022
Nipashe




Mbappe aelezea furaha kusaini PSG UKURASA 21

NACHOMOA...



Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (mwenye rasta), akiifungia timu yake bao la kusawazisha wakati ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Geita Gold FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YASOGEZA UBINGWA YANGA

●●● Yahitaji pointi nne tu kubeba ndoo, ni baada ya Wekundu wa Msimbazi kuambulia sare Kirumba...

**Na Adam Fungamwango**

NI wazi kabisa kuwa siku za kuutema ubingwa kwa Mabingwa Watetezi, Simba zinahesabika baada ya jana kulazimisha tena sare ya bao 1-1 dhidi ya Geita Gold FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

**Matokeo hayo yanaifanya Yanga sasa kuhitaji pointi nne tu katika mechi zake tano zilizosalia ili kufikisha alama 67 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote kati ya 16 zinazoshiriki ligi hiyo msimu huu.**

Simba iliyopo nafasi ya pili ikiwa na alama 51 zilizotokana na mechi 25, hata kama ikishinda michezo yake mitano iliyosalia itafikisha pointi 66 ambazo alama moja nyuma ya Yanga endapo itavuna pointi nne tu katika mechi zake tano.

Kwenye mechi hiyo ya jana, straika George Mpole ameongeza bao na kufikisha jumla ya mabao 14 akiongoza kwa muda dhidi ya mpinzani wake mkubwa, Fiston Mayele wa Yanga mwenye mabao 13, kabla ya mechi yao ya leo dhidi ya Biashara United itakayopigwa Uwanja wa CCM Kirumba.

Katika mchezo huo Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco alionekana kuifikiria zaidi mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA, Jumamosi wiki hii dhidi ya Yanga, kwani aliwapumzisha baadhi ya wachezaji wake muhimu kama kipa namba moja, Aishi Manula na beki wa kati, Henoc Inonga, huku akimwingiza kipindi cha pili Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Beki wa kulia Shomari Kapombe aliumia mapema kipindi cha kwanza na nafasi yake kuchukuliwa na Jimson Mwanuke.

Iliwachukua Simba sekunde 25 tu kupiga hodi kwenye lango la Geita Gold kwa Msenegal Pape Sakho kupiga shuti kali akiwa nje ya eneo la hatari ambalo lilipanguliwa na kipa Khomeini Aboubakar na kuwa kona.

Mabeki wa Simba walimsahau Mpole dakika ya 13 na kumpa nafasi ya kupiga shuti akiwa karibu kabisa na lango, mpira ukatoka sentimeta chache, huku kipa Beno Kalolanya akiwalaumu mabeki wake.

Ilimchukua dakika sita baadaye straika huyo kuiandikia Geita Gold bao la kwanza, likiwa la 14 kwake msimu huu, baada ya kutokea purukushani kwenye lango la Simba.

Alikuwa ni Offen Chikola aliyeambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto na kupiga krosi iliyopigwa na Edmund John iliyoleta kizaazaa kwenye lango la Simba, ikawa piga nikupige kabla ya kumfikia mfungaji aliyekwamisha wavuni.

Nusura Geita Gold ipate bao la pili dakika ya 25 kama shuti kali la Offen Chikola lililompita kipa Kakolanya, kugonga mwamba wa juu na kurejea uwanjani.

Mchezaji aliyesajiliwa na Simba msimu huu akitokea Mbeya City, Kibu Denis alisawazisha bao dakika ya 27, baada ya kuunganishwa kwa kichwa kona iliyochongwa na Rally Bwalya na kumfanya kufikisha bao la saba msimu huu. Ni kona iliyopigwa nje kidogo ya lango, ikamkuta Kibu ambaye alipiga kichwa cha nguvu kilichokwenda wavuni, licha ya jitihada za beki mmoja wa Geita Gold kutaka kuokoa.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, Simba ikiwatoa nahodha John Bocco ambaye hakuwa na mchezo mzuri, Gadiel Michael na Thadeo Lwanga na Sadio Kanoute, nafasi zao zikichukuliwa na Meddie Kagere, Peter Banda, Tshabalala na Erasto Nyoni.

Geita Gold iliwatoa Chikola, na Raymond John, huku Amos Kadikilo na Raymond Masota wakichukua nafasi zao, lakini mabadiliko hayo hayakuweza kubadili ubao wa matokeo uwanjani hapo. Geita Gold nayo imepanda hadi nafasi ya nne ikiwa na pointi zake 35.

## Nabi aanza msako usajili mpya Yanga

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikiendelea kupambana kuhakikisha wanapata matokeo katika michezo mitano iliyosalia ukiwamo wa leo dhidi ya Biashara United, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi, ameanza hesabu za kujenga kikosi imara kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa.

Yanga ambayo leo itashuka katika Uwanja wa CCM Kirumba kuvaana na Biashara United, inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 63 na kuwa miongoni moja ya timu ambayo hadi sasa ina tiketi ya kuiwakilisha nchini katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema yeye wakati yupo kwenye kusaka matokeo, viongozi wa klabu hiyo wanaendelea na mchakato wa kufanyia kazi mapendekezo aliyowapa awali katika usajili wao kwa msimu mpya.

Alisema kikosi cha Yanga msimu ujao kitakuwa na makali zaidi kwani kuna mambo ya msingi kiufundi msimu huu hayakwenda vizuri kutokana na sababu zilizopo nje ya uwezo wake.

"Yanga ya sasa mbali ya kuonekana kuwa kali, bado haijafikia nilipokuwa nahitaji kuona inakuwa tishio ndani ya uwanja, licha ya kupata matokeo mazuri katika ligi, lakini bado ninahitaji kikosi kijacho kuwa hatari zaidi," alisema kocha huyo.

Alisema licha ya kuwa na kibarua kikubwa cha kuhakikisha wanapambana kushinda michezo yao yote iliyobaki, lakini pia yuko makini katika suala la kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao kwa ajili ya kuanza mapema maandalizi ya msimu mpya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >